# UMAANISHO KATIKA TAMTHILIA YA *MAMA EE* YA MWACHOFI

**NA**

**EUNICE ALIVITSA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA MASOMO YA KISWAHILI, IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2017.**

**UNGAMO**

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kingine chochote, kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Eunice Alivitsa

(C50/72424/2014)

Sahihi:................................................................ Tarehe:................................................................

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Nairobi.

Prof.: John Habwe

Sahihi:..............................................................Tarehe:...................................................................

Bi.Mary Ndung'u

Sahihi:……………………………………………Tarehe:…………………………………………

## TABARUKU

Kwako wewe mama yangu mpendwa: Agneta Ambogo Amiani, aliyenilea, kunielekeza na kunishauri kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto za maisha, na kwenu nyinyi wanangu wapendwa Lean Ambogo na Bravin Kedeng'e mlivyonitia hamu ya kuendelea kuishi na kuzikabili pandashuka za maisha kwa ujasiri.

# SHUKRANI

Mchakato mzima wa kuikamilisha tasnifu hii haukuwa kwa bidii zangu mwenyewe bali iliweza kufanikishwa kutokana na michango na msaada wa wengine. Kwanza kabisa ninamtolea Mwenyezi Mungu kwa fadhili zake na kunipa nguvu za kukabiliana na changamoto mbalimbali wakati nikiitafitia mada hii. Mwenyezi Mungu pia aliweza kunipa hamu ya kuendelea na kutokata tamaa wakati wa kufanya utafiti huu hasa pale nilihisi kulemewa na changamoto za maisha. Kwa hivyo sina budi kumtukuza na kumheshimu kila wakati. Pili natoa shukrani zangu kwa wasimamizi wangu Prof. Habwe na Bi. Mary Ndung'u kwa kuniongoza na kunielekeza katika kuiandaa kazi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa hakika mmeniongoza na kunifanya kujifunza mengi kuhusu utafiti huu. Msingenielekeza, kwa kweli ingekuwa vigumu kufanya utafiti huu. Asanteni sana kwa uvimilivu wenu kwangu katika kunikosoa na kunielekeza hadi nikafika kiwango hiki. Shukrani sana na Mungu awabariki.Vilevile, ningependa kutoa shukrani zangu kwa wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi, idara ya Kiswahili. Mafunzo na ushauri wenu ndio ulionipa motisha na hamu ya kuifanya kazi hii na kuikamilisha, nawashukuru nyote na Mwenyezi Mungu awabariki kwa kazi nzuri mnayoifanya.Mwisho, ningependa kuwashukuru rafiki zangu wa dhati ambao wameweza kupitia mkondo huu kwa ushauri wao kwangu. Waliniongoza na kunishauri hadi mahali hapa nimefika. Nao ni pamoja na Pamela Alekana, Braicy Inziani na Gladys Kinyua. Hakika mmekuwa rafiki zangu wa karibu mmefaa kila wakati nilipohitaji usaidizi wenu. Mungu awabariki na muendelee na moyo uo huo.

## IKSIRI

Utafiti huu umeshughulikia Umaanisho unavyojitokeza katika tamthilia ya *Mama ee.* Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975) na kujikita katika kanuni nne za utaratibu wa ushirikiano. Data ya uchunguzi huu ilitokana na uchambuzi wa matumizi ya lugha na matamshi ya wahusika katika tamthilia ya *Mama ee.* Katika kufanya hivyo mtafiti alichunguza ni kwa kiasi gani kanuni za utaratibu wa ushirikiano zilivyokiukwa na hivyo kuzua umaanisho. Lengo la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha iwapo umaanisho unajitokeza katika *Mama ee*. Lengo hili lilitimizwa kwa kujikita katika matumizi mbalimbali ya lugha na kubaini kuwa katika matumizi hayo ya lugha yameweza kuibua umaanisho na hali hii inajitokeza pale ambapo kanuni za utaratibu wa ushirikiano zinapokiukwa. Lengo la pili lilikuwa, kuchunguza jinsi kanuni za utaratibu wa ushirikiano zinavyodhihirika katika ujenzi wa wahusika katika *Mama ee.* Katika kuvunja hizo kanuni sifa mbalimbali za wahusika zinajitokeza. Wahusika ili waweze kuendeleza mawasiliano hawana budi aidha kuzingatia au kukiuka kanuni za utaratibu ushirikiano. Jambo hilo limechunguzwa na kuweza kumsawiri kila muhusika na uhusika wake katika tamthilia ya *Mama ee.*Vilevile uchunguzi huu ulidhamiria kuchunguza umaanisho katika kukuza maudhui katika *Mama ee.* Matokeo yanaonyesha kuwa kukiukwa kwa kanuni nne za utaratibu wa ushirikiano na wahusika katika *Mama ee* kunaweza kukuza maudhui mbalimbali katika tamthilia ya *Mama ee.* Kwa ujumla, utafiti huu umebainisha kuwa, umaanisho una nafasi kubwa katika kuihakiki na kuikamilisha kazi nzima ya tamthilia. Kupitia uchunguzi huu, imethibitika kuwa, kufanikiwa kwa maingiliano ya wahusika katika tamthilia kunategemea kiwango chao cha kukiuka au kuzingatia kanuni nne za utaratibu wa ushirikiano ili kuendeleza mazungumzo yao. matokeo ya utafiti huu ni kuwa nadharia ya Umaanisho kwa kiwango kikubwa imeweza kutumika katika uchambuzi wa kazi ya fasihi hasa tamthilia ambayo msingi wake umejengwa kwenye mawasiliano. Mapendekezo ya utafiti huu ni kuwa kwa sababu ya kutokua na muda wa kutosha, watafiti wengine wajitokeze na kufanya utafiti zaidi wa wahusika, maudhui na matumizi ya lugha katika riwaya na hadithi fupi.

## YALIYOMO


Ungamo ..... ii

Tabaruku ..... iii

Shukrani ..... iv

Iksiri ..... v

Yaliyomo ..... vi


## SURA YA KWANZA


Utangulizi ..... 1

1.1 Usuli wa Mada ..... 1

1.2 Kuhusu Tamthili ya *Mama ee* ..... 4

1.3 Tatizo la Utafiti ..... 5

1.4 Maswali ya Utafiti ..... 5

1.5 Madhumuni ya Utafiti ..... 6

1.6 Sababu za Kuchagua Mada ..... 6

1.7 Upeo na Mipaka ..... 8

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..... 8

1.9 Msingi wa Kinadharia ..... 13

1.9.1 Jinsi Ukiushi wa Kanuni za Utaratibu wa Ushirikiano Katika Mawasiliano Unavyojitokeza ..... 16

1.9.1.1 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Idadi ..... 16

1.9.1.2 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Uhusiano. ..... 16

1.9.1.3 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Jinsi/ Namna ..... 17

1.9.1.4 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Ukweli. ..... 17

1.10 Mbinu za Utafiti ..... 17

1.10.1 Uteuzi wa Sampuli ..... 17

1.10.2 Ukusanyaji Data .... 18
1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data .... 18

**SURA YA PILI**

**UKIUSHI WA KANUNI ZA UTARATIBU WA USHIRIKIANO KATIKA MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI**

2.1 Utangulizi .... 20
2.2 Matumizi ya Sitiari .... 20
2.2.1 Mama ee ni Majuto .... 22
2.2.2 Ndoa ni Jela .... 23
2.2.3 Fimbo ni Adhabu .... 23
2.2.4 Pingu ni Minyororo .... 23
2.2.5 Watumwa ni Wanawake .... 24
2.2.6 Msalaba ni Majukumu .... 24
2.3Matumizi ya Methali .... 24
2.4 Matumizi ya Tashbihi .... 30
2.6 Matumizi ya Majazi .... 34
2.7 Misemo na Nahau .... 36
2.8 Mbinu Rejeshi .... 41
2.9 Kejeli .... 41
2.10 Maswali ya Balagha .... 43
2.11 Kinaya .... 44
2.12 Chuku .... 44
2.13 Hitimisho .... 45

## SURA YA TATU

## UKIUSHI WA KANUNI ZA UTARATIBU WA USHIRIKIANO ZINAVYOSAIDIA KATIKA UJENZI WA WAHUSIKA

3.1 Utangulizi ........ 46

3.1.1 Ukiushi wa Kanuni ya Idadi ........ 46

3.1.3 Ukiushi wa Kanuni ya Uhusiano ........ 49

3.1.3 Ukiushi wa Kanuni ya Ukweli ........ 53

3.1.4 Ukiushi wa Kanuni ya Namna/Jinsi ........ 56

3.1.5 Hitimisho ........ 60

## SURA YA NNE

## UMAANISHO KATIKA UKUZAJI WA MAUDHUI

4.1 Utangulizi ........ 61

4.1 Umaanisho na Ndoa. ........ 61

4.3 Umaanisho na Utamaduni ........ 64

4.4 Umaanisho na Ubaguzi wa Jinsia ya Kike ........ 65

4.5. Umaanisho na Dini ........ 67

4.6 Umaanisho na Ushirikiano wa Kina Mama ........ 69

4.7 Hitimisho ........ 70

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi ........ 72

5.2 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti ........ 72

5.3 Mapendekezo ........ 74

5.4 Hitimisho ........ 74

**MAREJELEO** ........ 75

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Taswira ya utanzu wa tamthilia nchini Kenya na Tanzania imechukua mikondo tofauti tofauti. Hii ni kutokana na mabadiliko mengi ambayo imeweza kupitia. Mabadiliko hayo yanachukua mikondo mitatu. Mkondo wa kwanza ni zile tamthilia zilizoandikwa kabla ya uhuru, tamthilia za wakati wa uhuru na zile zilizoandikwa mnamo mwanzo wa miaka ya 1980 hadi sasa. Mabadiliko hayo yanatokana na mabadiliko ya masuala ibuka yaliwaongoza waandishi kuweza kuandika kazi zao. Haya ni kulingana na Mulokozi M. (1996)

Hapo awali kabla ya mwambao wa Pwani ya Afrika mashariki kuingiliwa na athari za kigeni zilizotoka ng’ambo, fasihi ya Kiswahili ilikuwa ya kusimuliwa tu. Mifano ya tanzu hizo K.V ng’ano, vitendawili na methali zilihusishwa. Tangu mwaka wa 1953 tamthilia nyingi zimewahi kutungwa na kuchapishwa nchini Kenya na Tanzania, huku wahakiki wengi wakijitokeza kwa wingi. Taswira ya utanzu wa tamthilia haikuwa kama ilivyo sasa. Kwa sababu palikuwa na maigizo ambayo yalitolewa mbele ya hadhira kwa minajili ya kuongoa na kufundisha maadili au hata kutoa sifa kwa vitendo mwafaka vya wanajamii husika.

Wageni walipowasili (Waarabu na Wakoloni), maonyesho haya yalitoka kwenye mkondo wa kuigiza katika maandishi na kuiga mitindo ya kimagharibi. Ili kuchukua mkondo wa tamthilia kwa jumla kihistoria, tamthilia ilianza kutongoa maudhui ya kidini ambayo yalihusisha uteuzi wa matukio fulani kutoka katika kitabu kitakatifu cha Bibilia ili kutoa funzo fulani. Mabadiliko yalipoendelea kutokea katika maisha ya mwanadamu, hali hii ilibadilika hadi kuingia katika tamthilia zilizozingatia maudhui mengine kama vile vichekesho na tanzia. Katika karne ya kumi na sita (16) hata hivyo msisitizo ulitoka katika dini na kuigiza masuala ya kijamii, kwa hivyo tamthilia zikaanza kuzingatia maadili ya kijamii na kisiasa. Maudhui katika tamthilia ya Kiswahili huwasilishwa kimazungumzo kupitia kwa njia ya utendaji ambayo hufanywa kwenye jukwaa, kutazamwa kwenye runinga na kusikilizwa kwenye redio. Kuna yale ambayo hufanikisha kuwasilishwa kwa maudhui. Haya ni pamoja na taarifa ya kisanaa, uhusika, visaidizi, maelezo ya jukwaa, miondoko, ploti, maana na mgogoro na hadhira.

Katika mawasiliano hasa ya kimazungumzo kama ilivyo katika tamthilia ya *Mama ee*, huwa kuna msemaji ambaye amebeba ujumbe anaolenga kuwapasha pengine msikilizaji au wasikilizaji. Jambo hili ni la muhimu katika kumwongoza mwandishi kuweza kupasha ujumbe wake kwa wasomaji wa kazi yake. Katika kuandika kazi yake ya tamthilia, lazima aweze kupanga maudhui na kuwateuwa wahusika ambao watasaidia kujenga maudhui hayo na kazi yote kwa jumla. Mazungumzo katika tamthilia ni baina ya wahusika ambao watasaidia msomaji kuweza kupata lengo la mwandishi wa kazi hiyo.

Mzungumzaji ndiye huwa amelibeba jukumu la kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji. Msikilizaji kwa upande mwingine huwa jukumu lake ni kupata fasiri bora ya ujumbe huo kulingana na jinsi atakavyonena msemaji. Ni muhimu katika mawasiliano yoyote mtu kuchagua maneno na pia njia bora ya kuwasilisha ujumbe wake ili kumfanya msikilizaji kupata alicho maanisha kwa njia rahisi.

Mazungumzo yoyote hutumia lugha, iwe ni lugha ishara au lugha ya mazungumzo. Lugha katika mawasiliano huwa na majukumu ambayo kuendeleza shughuli mbalimbali za kijamii K.M za kibiashara, za kiuchumi na kusaidia wanajamii kuingiliana na kuleta utangamano katika jamii.

Kwa mujibu wa Grice (1975) ambaye ni mwaasisi wa Nadharia ya Umaanisho katika jukumu la kwanza la kuendeleza shughuli mbalimbali za kijamii, la mno ni kufikisha ujumbe kwa njia ya moja kwa moja ili kuafikia hatima ya jambo fulani. Kwa mfano, kama ni mazungumzo ya kibiashara, muuzaji na mnunuzi ni lazima waweze kuafikiana kwa njia ya mawasiliano. Katika kufanya hivyo kanuni ya idadi lazima izingatiwe. Muuzaji lazima aseme kikamilifu bei ya bidhaa zake ili mnunuzi apate kununua. Ikiwa muuzaji atasema kwa mfano "bei ya bidhaa hizi tutaelewana tu" atakuwa amevunja kanuni ya idadi na pale atamfanya mnunuzi asipate kuelewa anachomaanisha, katika jukumu la pili la kusaidia wanajamii kuingiliana na kutangamana, ni muhimu kuzingatia kanuni zote nne za mawasiliano. Kwa mfano lazima msemaji, azingatie idadi asiseme yanayozidi au yaliyopungua ila alenge tu yale anayoyasema. Pia, aweze kusema kwa namna ya kumfanya msikilizaji kupata anachomaanisha.

Mwisho, kanuni ya uhusiano na ukweli zizingatiwe. Katika kufanya hivyo kutakuwa na kuelewana. Lakini kwa upande mwingine kanuni hizi huvunjwa kwa kusema ukweli wa maneno fulani au pia kuhusiana na muktadha na hapo ndipo umaanisho unaibuka.

Kulingana na Crystal (2003) anataja vipengele vitatu muhimu vya kuzingatiwa na mzungumzaji anapotoa ujumbe wake. Mambo aliyotaja ni mada ya ujumbe, aina ya hadhira na mahitaji ya hadhira, Crystal (2003) anaendelea kusema kuwa mzungumzaji hawezi kutumia mtindo mmoja wa mazungumzo akizungumza na makundi tofauti ya watu. Mzungumzaji ni lazima aelewe mahitaji ya hadhira yake anapotumia lugha. Mambo anayoyazungumzia Crystal (1969) yatatufaa katika utafiti wetu kwa sababu yanachangia ufasiri wa ujumbe na msikilizaji ili kufikia maana ya msemaji ambacho ndicho kiini kikuu cha utafiti huu. K.M tukirejelea kauli ya Crystal (2003) inayosema kuwa mzungumzaji hawezi kutumia mtindo mmoja wa mazungumzo akizungumza na makundi tofauti, kauli hii itatufaa sana.

Hii ni kwa sababu niliweza kuona wazungumzaji wanavyobadilisha mitindo yao kimazungumzo kwa mfano wakati Mwavita na Kinaya wanapogombana itakuwa tofauti na vile wanavyozungumza mbele ya wazazi wao wakitaka ushauri.

Kwa upande mwingine katika mazungumzo, kuna vile huwa ni changamoto kuupasha ujumbe kwa kuzingatia kanuni nne zilizomo katika utaratibu wa ushirikiano. Hapo basi utapata kuwa kuna vile hizo kanuni zitakiukwa ili kuweza kuleta utangamano mzuri na wanajamii. Pia katika kukiuka kanuni hizo mtu huwa anazingatia maadili ya jamii husika ili asije akavunjia wenzake heshima. Ili kuteua mambo ambayo msemaji anataka kusema, lazima azingatie mambo K.V mahusiano ya kijamii, matabaka, vyeo, wakati, umri, jinsi, kiwango cha elimu, mandhari, wahusika na tukio lenyewe. Hivyo basi ataelewa anachozungumzia na kuwafanya wasikilizaji kumuelewa vizuri bila tatizo. Ikiwa kwa mfano ni mazungumzo baina ya wakwe, lazima pawe na heshima hivyo basi kanuni ya ukweli na namna itavunjwa ili kudumisha uhusiano wao. Katika matanga pia, kanuni ya ukweli, idadi na namna zitavunjwa. K.M ikiwa mtu alikuwa mwenye mienendo mibaya, hayo hayatatajwa moja kwa moja. Mzungumzaji lazima atafute njia mwafaka ya kupitisha ujumbe huo bila kuwafanya wasikilizaji kutatizika katika kupata maana yake.

Katika utafiti huu ninanuia kuchunguza iwapo kanuni za umaanisho zimekiukwa au la katika tamthilia ya *Mama ee* ya Ari Katini Mwachofi.Tutajikita katika kuchunguza namna mwandishi huyu ametumia tamathali za usemi kama vile methali, tashbihi, tanakali za sauti na jazanda. Ninachunguza ni kwa nini ametumia tamathali hizo katika mazungumzo kati ya wahusika. Ninachunguza ikiwa matumizi ya tamathali hizi yanavyowakuza wahusika na kujenga maudhui

katika tamthilia hiyo. Tutachunguza kanuni hizo ambazo ni, ukweli, idadi, uhusiano na namna iwapo zitakuwepo na kile alitaka kuwasilisha ili kuzua umaanisho miongoni mwa wahusika.

### 1.2 Kuhusu Tamthili ya *Mama ee*

Tamthilia ya *Mama ee* (Mwachofi 1987) ni miongoni mwa tamthilia zilizoandikwa mnamo mwanzo wa miaka ya themanini (1980) na kuendelea hadi karne ya ishirini na moja. Waandishi wengi waliangazia masuala ya kisiasa na ya kijamii. Katika tamthilia hii, matatizo yanayokumba ndoa yamesawiriwa. Ndoa hii ni kati ya Mwavita na Kinaya. Kinaya ameamua kujitumbukiza katika ulevi na uasherati. Katika kufanya hivyo ameitelekeza familia yake huku akimwachia mkewe majukumu yote ya nyumba. Ni kutokana na hali hii ambako kunazuka mapigano makali kati ya Mwavita na Kinaya ndoa basi ikaishia kuvunjika. Kuvunjika kwa ndoa hii ni baada ya Mwavita anayeashiria wanawake watumwa katika ndoa kuchukia msimamo mkali wa kutonyanyaswa hivyo basi akaamua kuishi peke yake bila mateso ya ndoa. Kwake Mwavita ndoa ni jela iliyojaa mateso dhidi ya mwanamke.

Mwachofi ni mwandishi ambaye ameweza kusawiri matatizo yaliyomo katika taasisi ya ndoa katika jamii. Ameweza pia kusawiri uhusiano wa kijinsia katika taasisi ya ndoa katika jamii yenye taasubi ya kiume.

Katika tamthilia ya *Mama ee* tunakumbana na matatizo katika ndoa ya Mwavita na Kinaya. Mwavita alipoolewa, mwanzoni hakufikiria ndoa ingegeuka ikawa vile ambayo mwanzoni ilikuwa ya kupendeza. Mwavita mambo yake yakaanza kwenda kombo akawa amezongwa na matatizo chungu nzima ya ndoa. Matatizo haya si mageni kwani hata sasa yanatokea katika jamii zetu.

Tenge dada yake Mwavita pia anapitia yayo hayo. Kwanza kabisa akapachikwa mimba, akafukuzwa shuleni ilhali George aliyempa huo uja uzito akakubaliwa kuendelea na masomo. Katika *Mama ee* kuna matabaka mawili yanajitokeza. Nayo ni  tabaka la wanyonge na tabaka la wenye nguvu. Tabaka la wanyonge linajipa moyo wa subira, kutia juhudi na kupinga unyonyaji, kutafuta uhuru, kuungana kudai haki, kujitegemea na kukataa kujitwika majukumu kupita kiasi, kukandamizwa, kupuuzwa na kupigwa yalitoka wapi:

### 1.3 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu umechunguza jinsi ambavyo umaanisho unavyojitokeza katika *Mama ee* na jinsi unavyosaidia katika kuwajenga wahusika na kukuza maudhui, ili kufanikisha drama, matukio na hadithi kwa jumla. Tafiti nyingi zimeweza kufanywa kuhusu umaanisho na umuhimu wake katika kudumisha mahusiano baina ya msemaji na msikilizaji wakati wa mazungumzo yao. Hata hivyo suala la umaanisho halijachunguzwa kwa kina katika kazi ya tamthilia na hasa katika fasihi ya Kiswahili ili kubainisha jinsi msomaji wa tamthilia huweza kubaini alichonuia mwandishi katika kuiandika tamthilia husika. Vilevile suala hili la umaanisho ikizingatiwa kuwa suala la muhimu katika mazungumzo halijaweza kushughulikiwa ili kuweza kubaini jinsi wahusika walivyojengwa kutokana na yale wanayosema. Haya yote ni masuala muhimu katika kuibua athari za kidrama kwa ujumla. Hii ina maana kuwa, tafiti nyingi ambazo zimefanywa zimekuwa zikijikita katika uchambuzi wa utanzu wa fasihi simulizi kama vile nyimbo na pia katika mazungumzo ya kawaida.

Baadhi ya tafiti hizi ni pamoja na utafiti wa Habwe J. (2011) ambaye aliweza kuchunguza suala la umaanisho katika mazungumzo ya kisiasa. Mtafiti huyu alijikita katika kuonyesha jinsi kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika mawasiliano ya kisiasa zinavyovunjwa. Hapa ni kwa kutaja tu chache. Ni kutokana na kuwepo kwa pengo hili la kutoshughulikia suala la umaanisho katika drama ya Kiswahili kwa kina ambapo utafiti huu unapata msingi wake. Swali ni je, Nadharia ya Umaanisho kwa kuzingatia mtazamo wa kipragmatiki inaweza kutumika kuchanganua lugha katika fasihi andishi hasa tamthilia? Katika kujibu swali hili utafiti huu umechunguza kanuni ambazo zinaongoza utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo baina ya muhusika na mwingine. Aidha ikiwa kuna utaratibu wa ushirikiano unajitokeza, matokeo yake ni yapi? Ni kutokana na maswali kama haya utafiti huu umechunguza jinsi nadharia ya Umaanisho inavyoweza kutumika kuchambua kazi ya fasihi hasusan ya tamthilia ya *Mama ee.*

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

i. Je, Umaanisho unajitokeza vipi katika *Mama ee*?

ii. Kanuni za utaratibu wa ushirikiano zinadhihirika vipi katika ujenzi wa wahusika katika *Mama ee?*

iii. Ni kwa jinsi gani kanuni za utaratibu wa ushirikiano zinakiukwa katika kukuza maudhui katika *Mama ee?*

### 1.5 Madhumuni ya Utafiti

Katika utafiti huu umaanisho umechunguzwa ili kutathmini matumizi ya lugha na ukuzaji wa wahusika na maudhui katika tamthilia ya *Mama ee.* Madhumuni yafuatayo yameongoza utafiti huu.

i. Kubaini umaanisho unavyojitokeza katika *Mama ee.*

ii. Kuchunguza jinsi kanuni za utaratibu wa ushirikiano zinavyodhihirika katika ujenzi wa wahusika katika *Mama ee.*

iii. Kubaini ni kwa jinsi gani kanuni za utaratibu wa ushirikiano zinakiukwa au kuzingatiwa katika kukuza maudhui katika *Mama ee.*

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Tamthilia ni sanaa ambayo huwasilisha mchezo wa kuigiza kwa njia ya maandishi na pia kuigizwa mbele ya hadhira. Katika kuchagua mada hii utafiti unanuia kuleta manufaa katika Kiswahili kwa ujumla. Kwanza kabisa matokeo ya utafiti huu yatakuwa na mchango kwa wasomi na watafiti wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Kwa mfano ni kupitia utafiti huu, watafiti wengine katika lugha ya Kiswahili watapata kichocheo na kupata mwelekeo wa kuchambua diskosi na kauli mbalimbali za wahusika katika kazi nyinginezo za fasihi kama vile riwaya, novela na hadithi fupi. Umuhimu mwingine ni kuwa utafiti huu utawanufaisha wasomi wa lugha ya Kiswahili katika kufahamu na kubainisha jinsi wanajamii mbalimbali huweza kuwasiliana kwa kujikita katika kanuni za utaratibu wa ushirikiano kwa kuzikiuka au kuzizingatia katika mazungumzo ili kufanikisha mawasiliano. Wataweza kubaini ikiwa ukiushi huu ni wa makusudi au ni wa kisadfa. Pia, utafiti huu utawasaidia wasomi wa Kiswahili na wanajamii kwa ujumla katika kutambua jinsi miktadha mbalimbali ya kijamii huathiri wanajamii katika kuzikiuka au kuzingatia kanuni nne za utaratibu wa ushirikiano wanapokuwa katika mazungumzo.

Mwisho walimu na wanafunzi wa vyuo vya viwango mbalimbali watanufaika na utafiti huu sana. Hii ni kwa sababu watapata fursa na maarifa zaidi ya jinsi ya kutambua sifa za wahusika katika

matini za fasihi pamoja na mchango wa hali mbalimbali za jamii katika kuathiri matumizi ya lugha ya wahusika. Vilevile wataweza kubaini dhamira ya mwandishi wa kazi ile hivyo basi kutaibuka na wengi ambao wataweza kuandika miongozo ya baadhi ya vitabu vya fasihi.

Sababu ya kuchagua tamthilia ya Mama ee ni kuwa tamthilia hii ni miongoni mwa tamthilia ambazo ziliandikwa katika miaka ya themanini wakati wa kuibuka kwa mitindo mipya ya uandishi wa tamthilia. Mwachofi aliweza kuibua masuala ya kijamii katika tamthilia yake. Ufundi wake wa kuteua wahusika, lugha na jinsi aivyokuza maudhui yake ni wa hali ya juu. Niliichagua kwa sababu hii ni tamthilia ambayo imetumika kama kisengere mbele. Hii ni kwa sababu yaliyotokea katika tamthilia hii yanafanana sana kwa kiasi kikubwa na matukio ya sasa katika familia za kisasa.

Hii ni kwa sababu miaka ya themanini hata kama wanawake waliweza kusoma, ilikuwa ni vigumu sana kutumia elimu yao kuweza kujinasua kutoka kwenye utumwa katika ulimwengu wa ubabe dume. Lakini Mwachofi aliweza kumsawiri mwanamke kama aliye na uwezo wa kujinasua kupitia elimu yake na kuweza kutekeleza majukumu ya wanaume. Tofauti na ilivyo na waandishi wa wakati ule hatuoni waandishi wakituonyesha ukombozi wa jinsia ya kike. Wengi wao wamesawiri mwanamke kama viumbe dhaifu vya kuteswa, kufungiwa na hata kutopewa nafasi ya kujitetea. Ufundi huu wa Mwachofi ndio ulinifanya kuteua kitabu hiki.

Sababu nyingine ni kwamba, mwandishi ameweza kutumia mbinu za sanaa katika hali ya fundi wa hali ya juu. Kwa mfano shairi la kwanza limetumika kama kisengere mbele kutuonyesha jinsi mambo kuhusiana na wanawake yatakavyokuwa katika tamthilia yenyewe na lile la mwisho limetumika pia kuonyesha maisha yalivyo baada ya mwanamke kujinasua kutoka kwenye tamaduni na mila za kuwadhalilisha. Hali hii ndiyo iliyonichochea kuweza kufanya utafiti na kuchunguza jinsi umaanisho unavyojitokeza katika kuwajenga wahusika na kukuza maudhui.

Kwa kuwa *Mama ee* ni tamthilia itanifaa sana katika utafiti huu kwa kuwa umaanisho huhusiana na jinsi mazungumzo yanavyojitokeza na kumfanya msikilizaji kuweza kupata maana lengwa ya msemaji. Hivyo basi tutapata kujua ni kipi mwandishi alichotaka kutupasha sisi wasomaji wa tamthilia hii. Alivyoweza kuwasawiri wahusika wake katika mazungumzo ni kwa jinsi gani waliweza kuelewana na hivyo kusaidia kukuza maudhui. Hapo ndipo tunapata kuwa nadharia ya umaanisho itatumika vizuri sana kuweza kuchambua kazi za fasihi haswa tamthilia. Sababu

nyingine ni kuwa katika kuchunguza tafiti zilizofanywa hapo awali kuhusiana na tamthilia ya *Mama ee* ziliweza kujikita katika nadharia za fasihi katika kufanya utafiti wao.

Data imechanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya Umaanisho. Tumeichagua nadharia ya Umaanisho kwa sababu ni nadharia ambayo inahusiana jinsi mazungumzo yanavyojitokeza na jinsi maana ya msemaji huteuliwa. Mikakati inayoongoza utaratibu wa ushirikiano ndiyo itakayotuelekeza kubaini ikiwa ilikiukwa au ilizingatiwa, hivyo basi kuzua Umaanisho wa masemaji. Tutaweza kubainisha jinsi tamadhali za usemi zinavyotumiwa kukiuka au kudhihirisha umaanisho ili kukuza maudhui na kujenga wahusika. Pia tutaweza kudhihirisha namna umaanisho unavyojitokeza miongoni mwa wahusika na kuangazia jinsi wahusika hao wanavyojengeka vilevile tutachunguza sababu ambazo huelekeza wahusika kuvunja kanuni za utaratibu wa ushirikiano hivyo basi kuibua Umaanisho.

**1.7 Upeo na Mipaka**

*Mama ee* ndiyo tamthilia iliyochaguliwa kama asili ya data ya utafiti huu utakuwa wa kiisimu katika kuchunguza fasihi ambalo ni somo maalum linalohusiana na tungo za sanaa kama vile tamthilia, riwaya, mashairi, misemo na vitendawili. Katika utafiti huu tunajikita katika uwanja wa fasihi andishi ambapo tunachunguza tamatishi. Nadharia ya umaanisho imetimika kudhihirisha nama tamthilia za usemi zikiwemo mbuni za lugha na mbuni za sanaa zinavyokiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano na hivyo kuzua umaanisho.

Umaanisho umetumika kuwasawiri wahusika kwa kuchunguza walivyokiuka na kuzingatia kanuni za utaratibu wa ushirikiano mwisho katika umaanisho umechunguzwa jinsi unavyokuza maudhui katika *Mama ee.* Tamthilia za usemi ambazo zimeshughulikiwa ni pamoja na sitiani, methali, tashbihi, kejeli, maswali ya balagha, kinaya na chuku.

Wahusika wote kwa jumla wameshughulikiwa na mwisho ni maudhui yafuatayo pia yameshughulikiwa maudhui ya ndoa, utamaduni, ubaguzi wa jinsia ya kike , dini na ushirikiano wa kina mama.

**1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Sehemu hii, imejadili yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Umaanisho na jinsi inavyojitokeza katika kazi mbalimbali. Pia yaliyoandikwa kuhusu Pragmatiki yameangaziwa hasa yale

yaliyolenga lugha mahususi ili kuchangia katika taaluma ya isimu. Kazi zilizofanywa kuhusu mawasiliano na matumizi ya lugha zilikuwa muhimu katika kutuongoza kufanya utafiti huu.Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa matumizi ya lugha hudhihirika katika muktadha maalum wa jamii na kuwa wakati wa mawasiliano ni muhimu kuzingatia muktadha. Katika kazi hii nitachunguza miktadha ambayo imetumiwa ili kuleta dhana ya Umaanisho katika tamthilia ya Mama ee na jinsi miktadha hiyo inavyoweza kuchochea matumizi ya lugha katika tamthilia hiyo.

Kulingana na Wamitila (2003), lugha ni chombo muhimu katika mawasiliano. Msemaji au mwandishi anaweza kuathiri mawasiliano iwapo atatumia lugha vibaya. Anasisitiza kuwa matumizi ya lugha ni kipengele muhimu cha kuchanganua jamii inayohusika. Kauli ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tutachunguza ni nini kilichomchochea Mwachofi K. kutumia lugha inayo kiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano hivyo kuzua umaanisho.

Trudgil (1983), anasema kuwa kila jamii ina sheria zinazoongoza matumizi ya lugha, mwingiliano na mtagusano wa wanajamii. Anasema katika mawasiliano,ni lazima mtu aelewe utamaduni wa jamii yake ili aweze kutumia lugha inavyotarajiwa. Katika kuelewa utamaduni huu, mtu ataweza kuongea ili asiweze kukiuka matarajio ya jamii. Katika Mama ee, kuna utamaduni ambao umo hatarini kutupiliwa mbali na mwanamke msomi kwa jina Mwavita anapojaribu kutetea jinsia ya kike. Hivyo basi kuna yale anakiuka kufuatana na utamaduni wa kitambo ili kuzuzua Umaanisho katika mazungumzo yake.

Lackoff (1976) anahusisha lugha na vitengo vingine vya jamii na kudai kuwa lugha pekee haiwezi kujitosheleza. Mtalaamu huyu anadai kuwa utafiti wowote wa kiisimu lazima ujikite katika kueleza sababu za watu kuongea jinsi wafanyavyo. Anadai kuwa maswala mengi katika lugha kama vile muktadha, sababu ya tamko au usemi fulani na jinsi ya kutafsiri usemi ni baadhi ya mambo ambayo hayajashughulikiwa kikamilifu. Kulingana na Lackoff (1976) sio sawa kuzingatia sintaksia pekee katika matini na kupuuza muundo ndani ya tungo. Ni muhimu kujiuliza ni kwa nini mzungumzaji anazungumza jinsi afanyavyo. Anatoa kauli kuwa si sawa kuwa na uamuzi wa jumla kwamba kila binadamu mwenye akili razini lazima atumie njia fupi anapozungumza. Anasisitiza kuwa ukamilifu wa maana hutegemea alichokusudia msemaji. Kauli hii ilinisaidia sana katika utafiti wangu kwa sababu nadharia ya Umaanisho inalenga hasa alichokusudia msemaji na hivyo basi ni kazi yake msikilizaji kuweza kuibuia maana lengwa ya

msemaji. Kwa vile ninashughulikia semi kauli hii ilitusaidia kuweza kupata fasiri za maana za semi hizo.

Habwe (2011) ameweza kushughulikia suala la umaanisho katika mazungumzo ya kisiasa. Ameonyesha kuwa kuna mambo ambayo huathiri kanuni nne za utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo. Mambo hayo ni pamoja na uheshimiwa; ambalo ni jambo linaloathiri sana kanuni ya uhusiano na upole. Kulingana na Habwe (2011), lugha inahusisha mamlaka, mbinu, kushawishi, kuhamasisha na kudhibiti yanayosemwa. Ni kutokana na hayo lugha yaweza pia kuhusisha mazungumzo yenye msimamo, jinsi ya kushirikiana na watu na kuwa na upole na mazungumzo mwafaka.

Masuala mengine ni kama vile ukweli, sitiari, maswali ya balagha, masimulizi, mazungumzo, katika hotuba ambayo huweza kuvunja kanuni za utaratibu wa ushirikiano na kuzuzua Umaanisho katika mazungumzo ya kisiasa. Aliweza kubaini kuwa kuna sababu ya kuvunja kanuni ya idadi, ukweli, uhusiano na jinsi miongoni mwa wanasiasa ili kuweza kujenga uhusiano mwema na wananchi wao. Kazi hii ilinifaa sana kwa sababu nilichunguza wakati tanakali za semi zinavyotumiwa huwa zinavunja kanuni gani na ni kwa sababu gani.

Utafiti uliofanywa na Ngoge (2012) kuhusiana na umaanisho, anadokeza kwamba nahau, kama kategoria ya kimuktadha pekee, mara nyingi huambatanishwa na kategoria zingine za kileksika ambazo huwa hazina maana funge kimazungumzo na ambazo zinaweza kuzua umaanisho vilevile. Mabadiliko ya muktadha ni suala ambalo husababisha mabadiliko ya maana. Hii ndiyo sababu kuu ya utafiti wetu kuchunguza jinsi miktadha mbalimbali zinavyozua umaanisho na kutusaidia kuona jinsi imesaidia kutafsiri wahusika na maudhui katika tamthlia ya Mama ee.

Pragmatiki ni taaluma inayoshughulikia maana ambazo zinahusiana na muktadha wa utumizi wa lugha. Katika pragmatiki muktadha unajumuisha msemaji, msikilizaji, mahali, wakati na mada ya mazungumzo. Chukulizi zisizo sahihi zinaweza kuzua umaanisho hasa miongoni mwa watu wanaotoka katika tamaduni na mazingira tofauti, na umaanisho wenyewe ukatokea kuwa sio ule uliokusudiwa. Hali hii ni kweli hasa ikizingatiwa kwamba miktadha hutofautiana kutoka kwa jamii moja hadi nyingine.Ogola,(2006). Hata hivyo chukulizi kama hizo zinaweza kuzuka miongoni mwa watu wanaozungumza lugha moja na kushiriki utamaduni mmoja kutokana na tofauti za umri, tofauti za mitazamo pamoja na ukosefu wa tajriba katika matumizi ya misimbo

inayozua umaanisho. Ni kutokana na kauli hii ndipo nilikusudia kufafanua zaidi jinsi umaanisho unavyoweza kutumika kufasiri wahusika katika Mama ee na jinsi unavyosaidia kukuza maudhui.

Katika tamthilia ya *Mama ee* (Mwachofi 1987) kuna kazi ambazo zimeshughulikiwa. Kazi hizo ni pamoja na kutathmini taswira ya mwanamke katika *Mama ee* na ya Chacha, (2013). Katika kazi yake Chacha, (2013) ameweza kushughulikia mambo ambayo yameweza kumchora mwanamke kama ambaye ni wa kuweza kupigana zaidi kuliko wanaume ikiwa ataamua. Mwavita amaeonyeshwa kuwa mwanamke wa kujifanyia yaote bila kusadiwa na mumewe. Katika kazi yake aliweza kutumia nadharia ya Sosholojia ya fasihi ya George, Lukas. Hii nadharia ya sosholojia hunuia kueleza sababu ambazo zimechangia kuibuka kwa kazi ya sanaa iliyo na umbo la kijamii. Kwa hivyo kulingana na kazi yake Chacha (2013) tunapata kuwa aliweza kutumia nadharia ya fasihi kuchanganua kazi ya fasihi.

Onyoni, (2012) ameweza kushughulikia usawiri wa wahusika wa kike katika tamthili za Natala na *Mama ee* kwa kutumia nadhari ya Ufeministi. Nadharia ya Ufeministi na ya Sosholojia ya fasihi ni miongoni mwa nadharia ambazo hutumiwa katika kuchanganua masuala ya fasihi. Swali ni je, nadharia ya Umaanisho kwa kuzingatia mtazamo wa Kipragmatiki inaweza kutumika kuchanganua maswala ya utanzu wa ufasihi andishi hasa tamthilia?

Hii ni kutokana na kanuni zake ambazo zinaongoza utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo. Suala hili la ushirikiano linajitokeza vipi baina ya mhusika na mhusika na wasomi na mwandishi.

Luciana na Patrick (2014) walichunguza uwepo wa umaanisho wa kimazungumzo katika matini. Walisema kuwa msomaji aweze kuona umaanisho wa kimazungumzo kama njia ya kujadili maana katika matini ya kimazungumzo. Katika utafiti wao waliweza kubaini kuwa matini na umaanisho wa kimazungumzo kwa kiwango kikubwa zinaingiliana. Katika utafiti wao waliweza kugundua umuhimu wa matini katika umaanisho wa kimazungumzo. Kazi hii ni muhimu sana kwani nilikuwa nikiteua mifano mbalimbali katika Mama ee ambayo ndiyo matini yetu na kutolea mifano ya jinsi umaanisho ulivyoibuka.

Blutner (1998) alichunguza lengo la pragmatiki leksika ni kueleza jinsi maana za kileksika hurekebishwa katika hali ya kimazungumzo. Hii ni muhimu kwa sababu katika mazungumzo, maneno hutumiwa katika njia ambazo hufanya maneno kwenda kinyume na maana asili za

maneno hayo, yaani maana yake ya kisarufi. Mawazo yake ni muhimu kwetu ambapo niliweza kuchunguza maneno yalivyotumiwa katika *Mama ee* kama vile kijazanda na kuweza kufafanua maana yake kwa kuzingatia ni kanuni ipi ya utaratibu wa ushirikiano iliyokiukwa.

Yule (2010) anaeleza kuwa lazima tutumiea maana za maneno, mazingira ambamo maneno hayo yanatokea na kuweza kutambua ni kipi kilimchochea mwandishi akapata kutoa ujumbe ule. Tafsiri za maana hazilengi tu maneno bali kile ambacho tunafikiria mwandishi alitarajia kuwasilisha. Hii ni ya umuhimu kwetu hivi kwamba tutaweza kuchanganua matumizi ya lugha katika *Mama ee* ka kuchunguza vile tamathali za semi zilivyotumiwa na kuweza kutafsiri alicholenga mwandishi kutupasha.

Njuguna (2010) katika kazi yake alitumia nadharia ya pragramatiki leksika ambapo aliweza kujikita jinsi msikilizaji hutafsiri maana iliyokusudiwa ya msemaji. Msemaji anafaa kupata maana kutokana na jinsi mzungumzaji anavyotumia lugha. Maoni haya yanachangia sana katika utafiti wangu kwa sababu nitakuwa nikitafsiri maana ya mwandishi Mwachofi katika Mama ee ili kuweza kuelesa jinsi umaanisho unavyojitokeza, unavyolenga wahusika na jinsi unavyokuza maudhui. Hii ni kutokana na jinsi mwandishi ameweza kutumia lugha katika tamthilia yake.

Okuku (2010) ameshughulikia uchanganuzi wa baadhi ya matini za Kiswahili akitumia mtazamo wa pragmatiki leksika. Katika kazi yake, ameshughulikia tamathali za semi akirejelea riwaya ya Kiswahili. Kazi hii ilinifaa kwani niliweza kubaini jinsi tamathali za semi zilivyotumika katika *Mama ee* huku nikitoa maelezo kwa msingi ya nadharia ya umaanisho. Kuna mwingiliano japo yeye alitumia riwaya huku mimi nikitumia tamthilia.

Gergely Bottya'n (1989) alichunguza nadharia ya umaanisho kwa mapana na marefu. Pia aliweza kuchunguza uwezekano wa kupima utendakazi wa nadharia hiyo ya umaanisho. Kwa kujikita katika kanuni nne za utaratibu wa ushirikiano. Alishugulikia sana umaanisho wa kimazungumzo ambao ni wa aina mbili. Kwanza ni wa kijumla na wa pili ni wa kipekee. Gergely anasema kuwa kuna tofauti kati ya umaanisho wa kijumla na wakipekee. Hivi kwamba katika umaanisho wa kipekee huhitajika vipengee vya kipekee katika matini ilhali umaanisho wa kijumla unahitaji utumiaji wa miundo fulani ya maneno katika matamshi kwa kawaida katika kutokuwepo kwa hali za kipekee, itabeba umaanisho wa namna hii au ile. Mfano wa umaanisho wa kipekee:

A. Yohana huenda hanywi pombe siku hizi.
B. Amekuwa ni vikao vya makundi ya kikanisa hivi karibuni.

Jibu la mhusika B limekiuka ushirikiano wa kimazungumzo umaanisho kuwa Yohana hanywi au yuanywa pombe na vikundo vya kikanisa ni muhimu. Hivyo basi B aiazingatia kanuni ya uhusiano. Georgely (1989) ametoa sifa za umaanisho wa kimazungumzo ambazo ni:

i) Umaanisho waweza kufanyiwa hesabu kwamba yaweza kupimwa kwa misingi ya kanuni za utaratibu wa ushirikiano, matamshi katika lugha, matamshi yasiyo ya lugha na yaliyo ya lugha, maarifa.
ii) Umaanisho wa kimazungumzo si ya kushikiliwa kutokana na matamshi kwa kubadili maneno yaliyotumiwa na visawe. Hii ina maana kuwa maneno yaliyo na maana sawa katika matini moja.
iii) Umaanisho wa kimazungumzo waweza kufutilia mbali maneno au matini Fulani pasipo na kuibua utata.
iv) Umaanisho wa kimazungumzo hautokani na kile kimesemwa bali ni kwa kukisema. Ni kutokana na kauli hizi muhimu ninapata kufaidika sana katika utafiti huu kwani nitaongozwa kutambua jinsi umaanisho umeibuka katika kazi yangu ya utafiti.

## 1.9 Msingi wa Kinadharia

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ya Umaanisho ambayo muasisi wake ni Grice P. (1975). Grice aliweza kugundua jambo la mawasiliano na maana yake. Hivi kwamba watu wakizungumza kuna maana mbili ambazo huibuka. Kuna maana ya lugha na maana ya msemaji. Grice alisema kuwa mazungumzo yoyote ya binadamu yanaongozwa na utaratibu wa ushirikiano ambao una kanuni nne.

Nadharia hii inabainisha uhusiano baina ya maana ya msemaji, maana inayotokana na vipashio vya sentensi na maana inayoibuka kulingana na maneno katika sentensi. Nadharia hii hushughulika na maana kulingana na msemaji. Kanuni za utaratibu wa ushirikiano ambazo huzua umaanisho ni pamoja na:-

i) Idadi
ii) Ukweli

iii) Uhusiano

iv) Jinsi/namna

Katika kurejelea kanuni nne za ushirikiano ambazo hufanikisha mawasiliano tutazifafanua kwa undani ili kubaini maana na matumizi ya kanuni hizo.

Kanuni ya idadi inasema kuwa msemaji anapaswa kusema yanayotosheleza na yasizidi kiasi wala kupunguza taarifa ili kuweza kuwasiliana kwa njia mwafaka. Habari inayosemwa yafaa iwe kamilifu. Kwa mfano mtu anaposema kupita kiasi maana ya yale anayosema haitajitokeza vizuri kwa sababu huenda yale yaliyosemwa hayaambatani na kinachozungumziwa na pale basi kutakuwa na utata. Vilevile anaposema machache yatamnyima msikilizaji kupata ujumbe ule kwani kutakuwa na vipengee ambavyo ni vya muhimu na ambavyo vimesahaulika hivyo basi kumfanya msikilizaji kutojua alichomaanisha msemaji. Hivyo basi ili kufikia maana lengwa, msemaji anafaa kusema maneno ya idadi kamili.

Kanuni ya ukweli inamtaka msemaji aseme kile kilicho cha ukweli. Habari zitakazotolewa na msemaji ziwe na ukweli na hivyo basi msemaji asiseme habari ambazo anaamini ni za uongo au habari ambazo hana uhakika nazo. Ikiwa msemaji atasema, basi ahakikishe anasema kile ambacho anaweza kudhibitisha. Aseme yale ana ushahidi nayo.

Kanuni ya tatu ni ya uhusiano inayomtaka msemaji atoe habari zinazohusiana na mada inayozungumziwa. Msemaji hakubaliwi kusema habari zilizoko nje ya mada au muktadha unaozungumziwa. Asiingize mambo yasiyohusiana na mada anayoshugulikia.

Kanuni ya mwisho ni ya namna au jinsi. Katika kanuni hii msemaji anapaswa kusema mambo yaliyo bayana, wazi na yaliyodhahiri bila kuficha chochote. Ujumbe usiwe na utata, uwe na mpangilio na utaratibu mzuri aidha uwe mfupi, lugha inayotumika pia lazima ieleweke na msikilizaji wake bila tatizo lolote.

Mawazo haya yanaafikiana na ya Malmkjaer (2004) anayesema kuwa kanuni za Grice zina uhusiano na sifa kadhaa za diskosi ambazo hutokana na ukweli kuwa kama mazungumzo yatakuwa na urazini basi lazima yawe na matamshi yaliyo na uhusiano. Kinacholeta uhusiano huu ndicho kinajulikana kama kanuni ya ushirikiano inayodai mzungumzaji atoe mchango wake kama unvyotakikana katika kiwango inapotokea, kwa lengo lifaalo na kwa kuegemea mwelekeo

unaotakikana katika mawasiliano. Anaendelea kusema kuwa ili kufaulu kutumia kanuni hii, wazungumzaji wanafaa kuzingatia vijikanuni vingine vinne vya idadi, ukweli, uhusiano na namna. Katika kanuni ya idadi, inayohusiana na idadi ya maneno ya ujumbe utakaotolewa, mzungumzaji aufanye mchango wake kuweza kufahamisha iwezekanavyo katika muktadha uliopo wa mazungumzo. Mzungumzaji asifanye mazungumzo yake yazidi yanayotarajiwa. Katika kanuni ya ukweli, mzungumzaji aufanye mchango wake kuwa wa kweli. Asiseme kile ambacho si kweli au kile asichokuwa na ushahidi nacho.

Nayo kanuni ya uhusiano inamtaka mzungumzaji kudumisha uhusiano. Asiyazungumze yale ambayo yatakuwa nje ya uhusiano uliopo. Kanuni ya nne ya namna inahitaji mzungumzaji kujali namna anavyosema aliyonayo. Aepukane na yale yasiyoeleweka, na yenye utata, aseme kwa kifupi na awe na mpangilio wa kile anachokisema. Kanuni hizi za Grice ni chukulizi na inatazamiwa msemaji atatoa yale yanayohusu kile kilichokusudiwa kwa njia iliyo wazi na yenye utaratibu, ni chukulizi pia kuwa wazungumzaji wanapozungumza watazingatia kaida hizi katika mawasiliano.

Kulingana na Grice, ikiwa mzungumzaji ataenda kinyume na kaida hizi kwa mfano kutopitisha ujumbe kama inavyotakikana, kusema uongo, kusema zaidi ya inavyostahili au pengine apotoke na msikilizaji asiweze kumwelewa kama inavyotakikana, basi itamfanya msikilizaji azue maana ambayo haikukusudiwa na kuzua utata. Umuhimu wa nadharia hii katika isimu unatokana na kweli kuwa pragmatiki hujihusisha na kuibua maana kulingana na msemaji. Hivyo ni maana inayotokana na maneno ya msemaji.

Katika mazungumzo utapata kuwa ni nadra sana kupata mzungumzaji akufuata kanuni hizi kila wakati anapoongea. Utapata kuwa mara nyingi kanuni hizi huvunjwa na zinapovunjwa ndipo umaanisho hujitokeza na upole. Akitoa mfano katika mazishis, kanuni ya ukweli huvunjwa ili kuzungumzia tu yanayokadiriwa kuwa ya ukweli kumhusu aliyeaga. Katika kufanya hivyo watakuwa wanazingatia matarajio ya kanuni ya idadi huenda ikavunjwa kutokana na cheo alichonacho mtu. Kwa mfano mtu ambaye anaheshimiwa katika sekta fulani, anapoongea hatakuwa na budi kupunguza maneno yake ili asiweze kushusha chini hadhi yake. Katika kufanya hivyo heshima yake itadumu. Katika kuandika barua pepesi, ujumbe mfupi au mukhtasari wa matukio fulani katika muktano, mtu atalazimika kupunguza ujumbe wake ili aweze kuwasiliana.

### 1.9.1 Jinsi Ukiushi wa Kanuni za Utaratibu wa Ushirikiano Katika Mawasiliano Unavyojitokeza

Kulingana na Darighgoftar na Ghaffari (2012) ukiukaji wa kanuni nne za Grice za mazungumzo huwa na habari pana kuliko vile zingezingatiwa. Kulingana na Thomas (1995) anasema kuwa mtu anaweza kuamua kuvunja sheria ya mawasiliano si kwa kukusudia kudanganya au kumpotosha bali ni kwa sababu anamchochea msikilizaji aweze kupata maana iliyo tofauti au maana zaidi na ile aliyosema.

Mey (1996) anasisitiza mawazo yake Thomas (1995) kwa kupeana maana inayoeleweka vizuri. Anasema kuwa kuvunja sheria kama njia ya mawasiliano kupitia njia ya mazungumzo ni wakati ule tunafanya kuvunja kanuni moja wapo ya zile nne ili kumwezesha anayezungumziwa kutafuta maana mbadala ya ile aliyomaanishwa.

#### 1.9.1.1 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Idadi

Huu ni wakati msemaji anatoa habari zaidi na yaliyotarajiwa au kidogo kuliko kiasi cha kawaida.

Mtu anapopigiwa simu na mwenzake akiomba usaidizi. Anayepigiwa simu akawa ameacha ujumbe kwenye mashine yake kuwa “Amini usiamini Juma hayuko nyumbani. Tafadhali wacha ujumbe baada ya sauti hii. Huenda niko nje au nitapokea simu. Ninaweza kuwa wapi? Amini usiamini, mimi siko nyumbani”

Msemaji huyu amesema mengi mno ambayo hayana msingi. Bila shaka ukiwacha ujumbe kwenye mashine yako ya simu, mtu atajua kuwa umetoka, kwa hivyo hamna haja ya kumuarifu kuwa hauko nyumbani.

#### 1.9.1.2 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Uhusiano

Ukiushi huu hutokea pale ambapo jibu la swali huwa haliambatani na swali liliulizwa.

Mzazi anapomuuliza mtoto wake jinsi alivyofanya katika mtihani wake baada ya shule kufungwa, naye mtoto badala ya kujibu, yeye akauliza kutaka kujua kitanza mbali cha runinga kiliko. Hapa inaashiria kuwa mtoto huyu pengine hakufanya mtihani wake vizuri ndipo hataki maswali kuhusu masomo shuleni. Hivyo basi anabadilisha mazungumzo ili yawe ya kumfaa wala sio kumuadhiri kimawazo.

#### 1.9.1.3 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Jinsi/ Namna.

Hutokea wakati ule ubayana, ufupi na uwazi katika mazungumzo hukosekana.

| | |
|---|---|
| Hussein: | Je,ningependa kukuuliza, utawania tena kiti cha Urais mwaka wa 2022? |
| Mwanasiasa: | Nimekwambia kuwa tuzungumzie ya sasa na kuhusu mwaka wa 2022, ningependa ujijazie. |

Kutokana na majibu ya mwanasiasa huyo inaonyesha bayana kuwa asingependa kuzungumzia suala hilo maana yake pengine kuna vile wamekubaliana na wenzake kwa hivyo asingeweza kuweka mwelekeo wake bayana ili asiweze kwenda kinyume na makubaliano yao katika mrengo ule.

#### 1.9.1.4 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Ukweli.

Hapa ni pale mzungumzaji anasema mambo yasiyoeleweka na ambayo hayana ukweli. Kama vile. Siku ya Krismasi, ambulensi ilimbeba mtu mlevi ambaye amezirai kando ya barabara. Punde si punde mlevi huyo akamtapikia yule daktari. Daktari akasema “Hoyee!, Hiyo ilikuwa siku yangu nzuri sana ya Krismasi.”

Kutokana na maneno haya, ukweli haujitokezi. Kwa sababu daktari hawezi kufurahia mlevi kumtapikia. Pia hakuna la mno la kufanya siku hiyo kuwa siku nzuri sana ya Krismasi.

## 1.10 Mbinu za Utafiti

Katika mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data zimefafanuliwa.

### 1.10.1 Uteuzi wa Sampuli

Katika utafiti huu nadharia ya umaanisho ya Grice (1975) imeteuliwa kuongoza ili kuchunguza namna wahusika katika tamthilia ya *Mama ee* wanavyotumia kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika kufanikisha mazungumzo yao. Tamthilia ya *Mama ee* ndio sampuli ya utafiti kwa sababu, tamthilia huhusisha lugha ya mazungumzaji ambapo wahusika husawiriwa wakizungumza kwa

njia ya moja kwa moja. Ni kutokana na haya, inakuwa ni rahisi kwa mtafiti kuchanganua jinsi kanuni za utaratibu wa ushirikiano unavyotumiwa na wahusika katika tamthilia ikilinganishwa na matini zinazohusisha lugha ya kinadharia.Wahusika wameteuliwa kulingana na mazungumzo yao miongoni mwao, kumetegemea usemi wa moja kwa moja kutokana na yale ambayo wahusika wanayasema tumeweza kuibua maudhui katika tamthilia ya *Mama ee.*

Kwa vile tafiti nyingi zimefanywa kuihakiki tamthilia ya Mama ee nyingi zimetumia nadharia za kifasihi. Hili ndilo jambo kuu ambalo limetuongoza kufanya utafiti huu.Kwa sababu tamthilia hii haijafanyiwa uhakiki wa kutumia nadharia ya kiisimu katika kuichambua, hivyo basi utafiti huu utakuwa wa kwanza na mchango mpya katika fasihi ya Kiswahili. Sababu nyingine ni kwamba mwandishi Mwachofi ameweza kutumia ustadi wa hali ya juu katika kuandika tamthilia hii hasa katika kusawiri wahusika na ujenzi wa maudhui. Hivyo basi ufundi wa mwandishi katika matumizi ya lugha katika tamthilia hii ni mojawapo ya sababu zinazonifanya, kuitumia katika utafiti huu.

Tutaweza kuwashughulikia wahusika wakuu na wasaidizi katika tamthilia hii kwa sababu wote wametumika kuibusha na kuyakuza maudhui mbalimbali. Hivyo basi wahusika hawa wanatangamana miongoni mwao katika tamthilia kwa mapana katika kukamilisha tamthilia hii, kifani na kidhamira.

### 1.10.2 Ukusanyaji Data

Katika ukusanyaji wa data, kwanza kabisa niliisoma tamthilia ya *Mama ee* na kuchunguza tamathali za usemi zikiwemo methali, tashbihi, isitiari, jazanda chuku na maswali ya balagha Nilizichuja tamathali hizo ili nisalie na zile hasa zitakazotumika kuonyesha Umaanisho unavyojitokeza katika tamthilia. Aidha nilichunguza mikakati ya Umaanisho ambayo ni ukweli, idadi, uhusiano na namna au jinsi zinavyokiukwa. Pia nilisoma tasnifu za wasomi wengine zilizoaandikwa kuhusu mada hii. Maudhui lengwa yalitambuliwa kutokana na mazungumuzo yao na muktadha ambamo mazungumuzo hayo yanatokea.

### 1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti huu pamoja na mihimili ya nadharia ya Umaanisho. Kwa kutumia mihimili ya nadharia hii nilichangua tamathali za usemi ambazo mwandishi kupitia kwa wahusika wakuu pamoja na wale wasaidizi wanatumia kudhihirisha

Umaanisho. Aidha niliweza kuchanganua iwapo ukiushi huu wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika mawasiliano umesaidia kuendeleza maudhui na hutokana na hali ya kawaida au huchochewa na muktadha wa mawasiliano.

Baada ya kukusanya na kuchanganua data, uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu ulifanywa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji huu ulihusu maelezo ya namna tamathali za usemi zinavyotumika kukiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano ili kuleta Umaanisho na katika kufanya hivyo kukuza maudhui na wahusika katika tamthilia ya *Mama ee.* Vilevile nilieleza iwapo Umaanisho katika mawasiliano huchochewa na hali ya kawaida au huchochewa na muktadha wa mawasiliano.

# SURA YA PILI

## UKIUSHI WA KANUNI ZA UTARATIBU WA USHIRIKIANO KATIKA MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI

### 2.1 Utangulizi

Katika sura ya pili utafiti unachunguza jinsi mwandishi wa *Mama ee* alivyoweza kutumia mbinu za lugha katika uandishi wake. Mwandishi wa kazi fulani au mzunguzaji anapotumia mbinu fulani katika kazi yake au mazungumzo yake huwa anakuwa na maana fulani ambayo haijitokezi waziwazi na ambayo yeye hutaka msikilizaji aweze kuitambua. Kwa mfano anapotumia methali huwa anataka maana fulani kulingana na kazi yake iweze kujitokeza. Hivyo basi methali haitakuwa ya maana ya moja kwa moja kama ilivyoandikwa katika kamusi za methali bali itakuwa na maana fiche ambayo ililengwa na mwandishi au msemaji. Katika *Mama ee* kama vile methali, isitiari, jazanda, majazi, mbinu rejeshi, tashbihi, kejeli, misemo, chuku, maswali balagha na kinaya zimetumika katika sehemu hii nimechunguza matumizi hayo ya lugha na kubaini ni kanuni gani ya utaratibu wa mawasiliano iliweza kuvunjwa au kuzingatiwa na sababu za kufanya hivyo.

### 2.2 Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo kwa mfano kitu, matendo au vitu vyenye sura mbalimbali hulinganishwa na hali sawasawa na maumbile au jinsi ya utendaji. Kulinganishwa huku huwa ni kwa moja kwa moja bila kutumia maneno "kama mfano", kama vile' 'ja' na "mithili ya". Sitiari ni dhana inayotokana na neno "sitiri" lenye maana ya kuficha au kufunika. (Kuhenga,1977, Wamitilia, 2003) Sitiari kama dhana inayoeleza sifa ya kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine. Maana huwa inamaanishwa kwa vile hakuna matumizi ya viungo.

Sitiari katika *Mama ee* zimetumika kuleta maana fiche ya msemaji ambayo msikilizaji au msomaji wa kazi ile anafaa kufanya juhudi ili kupata maana lengwa. Hivyo basi sitiari zinazua umaanisho. Wakati wa kuzitumia utapata kuwa ni maneno machache tu yanayotumiwa ilhali wakati wa kupata maana yake unapata kuwa maelezo ya maana ni mapana mno. Kwa kurejelea kanuni za utaratibu wa ushirikiano za Grice, kanuni ya idadi inavunjwa hivyo kumfanya msomaji au msikilizaji kuweza kuelewa maana yake. Kanuni ya ukweli pia inavunjwa kwa sababu kitu au mnyamna hufananishwa na mtu au kitu kingine. Hivyo basi msomaji au msikilizaji hana budi

kutambua sifa za kitu au mnyama yule ili aweze kuzifasiri na kuleta pamoja na kile kinachofananishwa ili kupata maana ya ndani. Kwa mfano:-

Ba mkubwa Kinaya: Ndiyo elimu ya siku hizi hiyo. Wamekuwa wazungu. Kama si wao kushika sana kizungu leo hii hatungeacha kazi zetu na kuja hapa.(uk 23)

Fungu hili la maneno… 'kuwa wazungu', halimaanishi watu kugeuza rangi na lugha yao wakawa wazungu. Alichomaanisha Ba Mkubwa Kinaya ni kuwa elimu ya kisasa, imewafanya wengi kuasi mila na desturi za hapo awali, wakaiga za uzunguni na kuwa kama wazungu ndipo matatizo mengi yanawakumba katika ndoa zao. Akisema hivyo alikuwa akiwaashiria Mwavita na Tenge ambao kila mara wanazozana na mzozo huo watokana nay ale waliyoyapata katika elimu zao. Kanuni ya ukweli imevunjwa kwa sababu maana ya sitiari hii ni kuwa watu kubadilika kwa kupata masomo ya kisiasa ya kuwafanya waasi mila na desturi.

Mwavita*:* Ati lazima nijidunishea mbele ya Kinaya na kuwa mvumilivu 'kike' ! Kwa nini niwe mvumilivu 'kike' kwani mke hana moyo? Mwili wake ni wa chuma? hasikii uchungu yeye?(uk 76)

Mwavita alikuwa anajutia yaliyompata akiwa katika ndoa. Inaonekana kuwa wengi hawakuwa wanaelewa aliyokuwa akipitia. Hivyo basi walikuwa wanamuona kuwa mwenye kiburi na maringo kwa sababu ya masomo yake na kazi yake. Waliona kuwa yeye ndiye anayeharibu ndoa yake. Hivyo alikuwa akiuliza mwanamke ni wa aina gani, je ana mwili kama wa chuma ambao huwezi hisi uchungu, unaweza stahimili makonde ya kila siku? Kwake akaona la hasha ni kiumbe sawa na vingine ambacho pia chaweza kutetea na kujitenga na uhasama wa ndoa. Hivyo basi hataweza kustahimili hayo. Kanuni ya namna iliweza kuvunjwa. Kwa sababu maana ya sitiari hii haiji moja kwa moja. Inamhitaji mtu kuweza kufanya uchambuzi ili aweze kuibua maana.

Mama: Awe kuja na ulimi wa sukari ukamkubali ati! Wanaume wajanja.(uk 80)

Baada ya Mama kumsikiza mwanawe Mwavita na yale aliyokuwa akipitia katika ndoa,basi aliweza kutambua kilichomfanya Mwavita kuamua kutoka katika ndoa yake. Mwavita alikuwa ameamua kuwa kamwe hatarudia Kinaya. Mama kusema kuwa huenda akaja na ulimi wa sukari, alimaanisha kuwa kwa kuwa wao wamejaa ujanja wa kujibadilisha leo mzuri kesho kageuka kuwa mnyama, Kinaya asije tena na maneno matamu yakumhadaa Mwavita ili aweze kumrudia. Ajiepushe kabisa na hadaa za Kinaya ambazo huenda zinaonekana nzuri mwisho zikawa za kumletea matatizo.

> Mwavita: Nilipokuwa mdogo nilidhani kuolewa ni mbingu ya saba kwa mwanamke.(uk 90)

Mbinguni ni kule kila mtu anatarajia kwenda baada ya kuiaga dunia. Huko watu hutarajia mema ya milele na milele wakifananisha na ulimwenguni ambao umejaa dhiki tele. Mwavita alidhani kuwa akiolewa basi atakuwa ameanza maisha yake ya raha mustarehe. Aliona kuwa maisha yatakuwa bora kuliko vile yalivyokuwa akiwa bado hajaolewa. Alipokutana na ukweli wa mambo ndipo aligundua kuwa si vile alivyodhania bali kwake ndoa ni kama jehanamu. Ambayo imejaa dhuluma, kupigwa, kuteswa, kuachiwa majukumu na matusi tele. Kanuni ya namna imeweza kukiukwa. Alivyosema Mwavita hakuleti maana ya waziwazi. Hivyo basi lazima utafute maana ya ndani kama nilivyoweza kuichambua. Baadhi ya sitiari nyinginezo zinazochunguzwa ni kama ifuatavyo:

### 2.2.1 *Mama ee* ni Majuto

Hii ndiyo anwani ya tamthilia hii. Katika anwani ya *Mama ee* tunapata kuwa kanuni ya ukweli imevunjwa kwa sababu ina maana ya ndani. Kwa mfano *Mama ee* ni maneno ambayo mtu akiwa hatarini au katika mateso huweza kusema kwa kutaka usaidizi au kuonyesha ana maumivu sana. Katika tamthllia ya *Mama ee,* wanawake ndio wanaoonekana kuwa katika mateso au katika kilio. Unapokumbana na anwani hii bila shaka inakupa taswira ya mchezo wote kwamba kuna vilio na majuto. Vilio hivyo tunaviona kwa Mwavita katika ndoa yake. Tenge alipopata mimba akiwa angali shuleni huku baba na kaka yake wakataka kumfukuza huku wakimchapa na mwisho ni mama yao anayeonekana kuwalilia watoto wake wa kike kwa sababu ya yale waliyokuwa wakipitia.

### 2.2.2 Ndoa ni Jela

Neno ndoa kwa kulinganisha na matukio katika *Mama ee* limetumika kijazanda. Lina maana ya ndani. Kulingana na Mwavita yeye anaona ndoa kuwa kama jela ya kufungwa. Mwanamke akakosa uhuru wake huku akinyanyaswa. Hii ndio maana anajutia kuolewa. Anaiona ndoa kuwa mahali pa mateso, pasipo na raha, palipo jaa huzuni na ambapo hapana uhuru. Badala ya kumpa raha mwanamke, inamdhalilisha na kumdunisha. Kwake Kinaya anachukulia ndoa kuwa ya kumtawala mwanamke kwa sababu ameshalipia mahari. Katika kulipa mahari, Kinaya anaona sasa amemnunua mwanamke na hivyo amtawale na kumwachia majukumu yote yakiwemo yale yanayokusudiwa kuwa ya mwanamume. Kwa vile neno hilo ndoa lina maana tofauti na ndoa ya kawaida, hivyo basi baada ya kufanya uchambuzi wa ndani tunapata kuwa kanuni ya ukweli na uhusiano zilikiukwa. Uhusiano umekiukwa kwa sababu hamna uwiano wa ndoa na jinsi vile Mwavita na Kinaya wanavyoiona.

### 2.2.3 Fimbo ni Adhabu

Katika tamthilia ya Mama ee neno fimbo limetumika wakati wa kumtoza Kinaya faini kutokana na yale aliyokuwa ametenda. Fimbo hapa haina maana na kiboko cha kumcharazia mtu. Lina maana ya adhabu atakayotozwa Kinaya kwa yale makosa aliyoyatenda. Mzee kijiji alipotumia neno hilo alikuwa anataka kuonyesha kuwa alikuwa akizingatia heshima akizungumzia mambo hayo. Hakutaka wapate makali ya neno adhabu. Hii inaonyesha ni mzee mwenye busara. Kutokana na ile heshima aliyopewa katika mkutano ule alikuwa hana budi kupima maneno yake hivyo basi kutumia neno fimbo. Kanuni ya idadi ilivunjwa kwa kutumia neno moja lililobeba maana pana na kuleta umaanisho ili uhusiano wa watu wale usiweze kuvurugika. Katika kufanya hivyo mzee kijiji akawa ameivunja kanuni ya namna ili asiweze kuwahuzunisha watu wake. Hatutaka kusema waziwazi kwani alihofia sana uhusiano usije ukavunjika.

### 2.2.4 Pingu ni Minyororo

Neno pingu limetumika na mama katika tamthilia ya *Mama ee*. Mama anapomwambia Mwavita kuwa atakapojitoa katika yale mambo yaliyomsibu akiwa katika ndoa ya kwanza, bila shaka atataka kufunga pingu za maisha akimaanisha kuwa ataolewa tena. Ni kutokana na maneno haya Mwavita atoa tafsiri nyingine tofauti ya upingu. Anasema kuwa “kweli nazo ni pingu. Wahenga walijua walipoziita pingu”. Mwavita alimaanisha kuwa pingu za maisha ni wakati unapoolewa na unakuwa kama mfungwa. Katika ndoa ile. Analichukulia neno hilo kumaanisha kukosa uhuru,

mateso na dhuluma dhidi ya mwanamke. Mwavita hapa anaivunja kanuni ya uhusiano kwa vile anatoa tafsiri nyingine tofauti ya pingu za maisha kando na ile tunayoifahamu.

### 2.2.5 Watumwa ni Wanawake

Watumwa ni watu ambao hawana uhuru, wanafanya kazi nyingi bila malipo, wanateswa kwa kupigwa, kunyimwa chakula na kunyimwa nafasi ya kutetea haki zao. Katika Mama ee neno watumwa linaashiria wanawake walio katika ndoa za mateso. Kwa mfano Mwavita katika ndoa yake alikuwa amejitwika majukumu yote ya nyumbani yakiwemo pamoja na ya mumewe. Licha ya kujitwika majukumu hayo, tunaona kuwa bwana wake haachi kumtesa kwa kumtusi na kumpiga hadi akaavya mimba mbili pasipo kutaka kwake Mwavita. Mwavita katika ndoa ile ajiona mtumwa kwa sababu anapotaka kujitetea anazuiliwa na dini, utamaduni na hata sheria ya nchi. Hapo ndipo anaamua na liwe liwalo na kujinasua asiwe mtumwa tena**.** Kwa sababu anatoa tafsiri nyingine ya neno "mtumwa" kando na ile ya kawaida ya watu walio matesoni, basi tunapata kuwa kanuni ya uhusiano imekiukwa kwani utumwa huwa hauhusishwi na ndoa.

### 2.2.6 Msalaba ni Majukumu

Kando na maana ya kawaida ya neno msalaba, kuna maana nyingine inayojitokeza katika tamthilia hii. Tunamwona Tenge akimzomea Padre kuhusu dini kwa sababu kulingana na Tenge Padre amejificha tu katika dini ili aonekane kuwa yeye ni mzuri. Anamkumbusha Padre walivyokuwa wakienda ulevini na Kinaya. Kwa kuona haya kuwa mambo yake yameanikwa wazi, Padre anajaribu kujituliza kwa kusema kuwa "huo ndio msalaba walioachiwa na Yesu Kristo". Katika kufanya hivyo kanuni ya ukweli ikawa imekiukwa kwa sababu alimaanisha kuwa hayo ndiyo majukumu wanayokabiliana nayo na kamwe hayatamshinda katu. Hivyo basi 'msalaba' lina maana kuwa majukumu waliyojitwika wakuu wa kanisa katika kutekeleza wajibu wao.

## 2.3Matumizi ya Methali

Methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbiwa au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa (TUKI,2004). Wamitila (2001) katika utangulizi wake anaeleza methali kama " msemo unaojitosheleza, wenye maana yenye nguvu na uzito, wenye muundo au sifa ya kishairi unaokusudiwa kuadhibu, kuelekeza, kuelimisha, kushauri na kadhalika." Arege na Nyanje

(2011) wamezieleza methali kama tungo, tajiriba, mafunzo pamoja na falsafa ya jamii. Methali pia hutumika kama mapambo au kukamilishia wazo katika tanzu nyingine za fasihi kama vile hadithi au mazungumzo. Ochichi (2013) katika mazungumzo ya kijamii, methali hutumiwa na wazungumzaji kwa nia ya kuipamba lugha kufupisha maelezo, keulimisha pamoja na kufahamisha. Methali hazitumiki tu kiholela ila mzungumzaji huteua methali itakayoafikia lengo la ujumbe alio nao na kuzua umaanisho atakaokusudia yeye msemaji. Hali hii hufanikisha mazungumzo kwa vile methali husimba maana zinazohitaji kufasiriwa kiumaanisho ili kufikia makundi ya mawasiliano.

Methali zinapotumia na mzungumzaji au mwandishi wa kazi yoyote ile, huwa hazijatumiwa tu kuipamba kazi ile bali pia huwa kuna maelezo ambayo hayajitokezi waziwazi. Hii ina maana kuwa masomaji lazima afanye uchunguzi wa kina ili kupata maana ya mwandishi. Katika kutumia methali bila shaka kanuni nne za utaratibu wa ushirikiano huwa zinakiukwa. Kwa mfano kanuni ya ukweli hukiukwa ili kuleta uelewano mzuri wa wasomaji au wanaozungumziwa. Mara nyingi methali hutumiwa kupunguza makali ya maneno ambayo yangetumiwa moja kwa moja. Kanuni ya idadi pia hukiukwa. Hapa tunapata kuwa methali moja iliyotumiwa huenda maana yake ya ndani ikawa na maelezo marefu na mapana sana hivyo kuwa ya idadi ya maneno kubwa ikilinganishwa na methali yenyewe. Kanuni ya namna pia hukiukwa. Methali hukiuka kanuni ya namna pale ambapo ukweli bayana ya mambo huwa haujitokezi waziwazi. Huwa hakuna maelezo ya moja kwa moja ya kauli hiyo.

Kanuni ya uhusiano pia huvunjwa kwenye methali. Hapa ni pale ambapo msemaji ameonelea kuwa yatakayosemwa yatawaathiri wasikilizaji na yatakuwa kinyume na matarajio yao. Basi pale mwandishi au msemaji atazungumzia yale ambayo hayako katika muktadha ule ili kudumisha heshima na utangamano mzuri na hadhira yake. Kuna baadhi ya methali ambazo zimetumika katika Mama ee. Hizo methali hazikupachikwa tu katika tamthilia bali zilitumika ili kuzua umaanisho. Kwa mfano:-

> Mama: Mabibi na mababu zangu mlionitangulia! Nimekosa nini kikubwa sana hata yote yanipate mimi? Tenge mwanangu nimekufunza siku nyingi. Dadako amekuonya na kukuonyesha mfano bora. <u>Kweli mwana msikivu haambiwi mchana kutwa</u>.(uk 14)

Mama anajutia yale ambayo anakumbana nayo kwa sasa. Kwanza kabisa ni kuteswa kwa Mwavita kwa kupigwa katika ndoa yake. Pili ni kufunzwa kwa Tenge shuleni baada ya kugundua kuwa ni mjamzito. Haya yote yakuwa juu yake mama. Hii hi kwa sababu lawama zote zitamwendea kwa kukisiwa kuwa hakuwafunza wanawe vizuri.

Katika methali hii mama alikuwa akimwambia mtoto wake Tenge baada ya kugundua kuwa amekuwa mjamzito na hata akafukuzwa shuleni. Hii ina maana kuwa Tenge alikuwa ameonywa mara nyingi bila ya kuwasikiza wakubwa wake. Hivyo methali hii ina maana kuwa Tenge alikuwa mkaidi asiyeambiwa akaambilika. Alikuwa ameonywa mara nyingi naye akawa hasikizi. Kanuni ya namna ikavunjwa kwa vile haileti maana ya moja kwa moja. Pia kanuni ya ukweli ikakiukwa kwa sababu ya mama kutotaka kuvunja mazungumzo yao.

Mama: Msumwue msumwue. Hayo ni majiyaliyomwagika.Yakimwagika hayazoleki mtamuua bure hamna mtakachopata.(uk 16)

Kulingana na mama alikuwa akiwaarifu mumewe na mtoto wake wa kiume kuwa hata wafanye nini Tenge, mambo yameshaharibika na hakuna kuyarekebisha tena. Wamwache wasimuadhibu. Alikuwa tayari amepata ujauzito na kufukuzwa shuleni. Kanuni ya idadi imekiukwa. Kwa sababu methali hiyo ina maneno machache ambayo yana maana pana ya kuweelezea baba na ndugu yake Tenge kuwa kwa kumwadhibu wanafanya kazi bure. Mambo yameshaharibika.

Mama: Huenda popote utaketi hapa hapa nyumbani. Leo atakayekupiga tanipiga mimi kwanza. Hilo nimeshaliweka. Kama utafukuzwa tutaenda sote, uchungu wa mwana kweli aujua mamake.

Mama alikuwa akimhakikishia Tenge kuwa kamwe hatamwacha hata kama amepatwa na msiba wa ujauzito akiwa bado shuleni. Kutokana na yale yote aliyoyapitia akimlea Tenge, hivyo basi mama haoni ni kwa jinsi gani atamwacha. Hii inaonyesha kuwa mama anaelewa zaidi anachopitia mtoto wake. Hapo basi kanuni ya idadi namna ikavunjwa kwa sababu kuna utata katika kuelewa alichomaanisha.

Mzee wa kijiji: Tusigombane wanangu.ulimi huharibu na ulimi

hutengeneza ukanyoosha iliyo kombo.(uk 27)

Mzee alitumia methali hii wakati wa Ba. Mkubwa. Kinaya na Ba mkubwa Mwavita walipokuwa wakiongea, ilionekana kuwa mazungumzo yao huenda yakazua ubishi. Hivyo mzee wa kijiji aliamua kutumia methali hiyo kuwaonya na kuwakashifu dhidi ya kurusha cheche za matusi ambazo huenda zikaharibu mambo yote badala ya kurekebisha. Hivyo basi kanuni ya ukweli ilizingatiwa kwa kuwaeleza kuwa wakiendelea kugombana huenda wakaharibu mengi.

Mzee wa kijiji: Tusiwashe moto na kuuchochea sasa, maana tumekutana hapa kuuzima. Kila mmoja wetu atakikana kuzijua na kuondoa hasira, wahenga walisema Hasira ni hasara. Hiyo ni kweli.(uk 29)

Mzee wa kijiji alipotumiwa methali hii, ilikuwa ya kumuonya Ba Mkubwa, Mwavita ambaye alikuwa amekasirishwa sana na vitendo vya kinaya. Mzee alimaanisha kuwa hasira zake hizo huenda zikaleta hasara kubwa badala ya kuleta mafanikio. Huenda hasira hizo zikafanya ndoa ya Mwavita kuvunjika kabisa badala ya kuwapatanisha. Huenda pia pande zote mbili ya Mwavita na Kinaya zikaambulia patupu. Kanuni ya ukweli na namna zikawa zimekiukwa.

Mzee wa kijiji: Mwavita umemsikia mumeo aliyesema na kukuomba msamaha. Unasemaje?maana yote ni juu yako. Sisi tukimsamehe haitafaa lolote maana hatuishi naye, wewe ndiye ujuaye taabu ulizopata. Wahenga walisema:kitanda usicholalia huwajui kunguni wake na wakaongezea pia kusema.adhabu ya kaburi aijuaye maiti mujibu mwenyewe mumeo.(uk 51)

Mzee alipotumia methali hizi alikuwa akimaanisha kuwa ni Mwavita tu ndiye anayeelewa mumewe na iwapo anasema ukweli au la. Pia alikuwa akimaanisha kuwa ni Mwavita anayeelewa vizuri mambo kumhusu mumewe na ndoa yao kwa ujumla. Kwani yeye ndiye aliye na ujumbe kamili. Anayoyapitia Mwavita katika ndoa na yale ambayo mumewe humtendea hayawezi

yakaelezwa na mtu mwingine ila Mwavita mwenyewe. Kwani wengine hawawezi kutambua hayo kwa **s**ababu hayawahusu. Kanuni ya ukweli imekiukwa. Kuna mengi ambayo yamefichwa katika methali hizi. Hivyo basi ili uweze kupata kilichomaanishwa lazima ufanye utafiti wa kiundani.

> Mzee wa kijiji: Hapo mke wangu ameeleza vizuri sana. Si nilisema mimi aisifuye mvua imemnyia! Au sivyo mwanangu! (uk 52)

Methali hii ilitumika baada ya Mwavita kusema, yale yote yanayomkumba katika ndoa yake. Kutokana na aliyoyasema, ilibainishwa kwamba ni ukweli mtu husema ukweli bayana kuhusu yanayomsibu kwani ni yeye tu anayeelewa yote anayopitia katika ndoa yake. Hivyo basi Mwavita alitoa ukweli bayana kuhusu matukio ya ndoa yao. Mzee hakutaka kuonekana kwamba anampendelea Mwavita, kwa sababu pande zote mbili zilifaa kutetewa kwa hivyo akawa amekiuka kanuni ya namna ili kuleta ushirikiano mzuri, baina yao.

> Mama: Po! Mungu ayapitishe mbali hayo (*Mwavita afuta machozi*) Pole mwanangu, Ndichi kilimwengu. Pole mamangu, mvumilivu, hula mbivu mwisho mambo yako yote yatakuja kukukalia vizuri. Kwako kukiungua jua kwa mwenzio kwateketea. Dunia uwanja wa fujo mama. Wako wenye taabu zaidi yako wewe poa mama!(uk 72)

Mama alipozitumia methali hizi, alikuwa akimhimiza mtoto wake Mwavita ili aweze kuwa mvumilivu katika ndoa na katika maisha kwani hakuna yale ambayo hayana mwisho. Hivyo basi baada ya dhiki yote atapata yaliyo mema. Mama anapomwambia Mwavita kuwa kwako kukiungua kwa mwenzio kwateketekea, alikuwa akimaanisha kuwa hakuna yeyote ambaye hapitii matatizo na huenda wale wengine wana matatizo makubwa sana kushinda yake Mwavita. Aliposema kuwa dunia uawanja wa fujo, alimaanisha kuwa hakuna pahali palipo pema duniani. Kila pahali pamejaa vurugu, uozo, vita na dhuluma za aina mbalimbali. Hivyo basi alikuwa akimtia moyo kuwa asiweze kudunishwa na ile hali aliyo nayo kwa wakati ule, bali aendelee kutafuta suluhisho la yale yanayomkumba. Methali hizo tatu zimebeba maana zaidi kuliko vile

zimeandikwa. Hivyo basi kuna ukweli ambao umefichika pia kuna kukiuka kanuni ya idadi na namna.

> Mwavita- (*Amrukia na kumnyoshea kidole*) wewe ambaye hujaoa utawezaje kunieleza mimi juu ya kuishi na bwana? Unajua nini juu ya maisha hayo? Aisifuye…………(uk 84)

Mwavita alipotumia methali hii alikuwa akimaanisha kuwa Padre ambaye hajoa kwa sababu za kidini anawezaje kuelewa mambo kuhusiana na ndoa hadi akawa wa kutoa ushauri kwa waliooana. Hivyo basi alikuwa akimaanisha kuwa Padre hajui chochote wala lolote kuhusiana na ndoa kwa hivyo hawezi kamwe kumpa ushauri. Kwa sababu hafahamu anachopitia Mwavita au walio katika ndoa. Mengi yamefichwa katika methali hii. Huenda Mwavita angemwambia ukweli bayana , basi angekuwa amevunja kanuni kuu ya mawasiliano ya utaratibu wa ushirikiano hivyo kukatiza mazungumzo.

> Tenge: Ndiyo mama mwambie. Mimi humwambia kuwa siku zote watu watatafuta la kusema. Jambo haliwahusu ndewe wala sikio, wao watalizungumzia tu.(uk 90)

Kanuni ya namna imeweza kuvunjwa kwa sababu kutokana na usemi huu, Tenge hajaweka bayana yale ambayo watu wanasema**.** Mwavita alikuwa amechoshwa na kusemwa na watu kuhusu ndoa yao iliyovunjika. Alikuwa hata amekataliwa na waliokuwa rafiki zake. Hivyo basi Tenge alikuwa akihimiza kuwa kamwe watu hawatachoka kusema. Hivi kwamba watasema hata na yale yasiyowahusu. Mama naye akamshauri kunyamaza. Tenge akitumia methali hii alitaka kumshauri Mwavita kuwa hakuna vile mtu atakosa kusemwa. Ila tu yeye anafaa kutupilia mbali wayasemayo na hivyo kuendelea mbele.

> Mama: Hata hivyo tazama yajayo Tenge. Ukikosea sasa itakuwa si kosa tena ni kusudi Msiba wa kujitakia.(uk 95)

Kanuni ya ukweli imekiukwa. Mama ana mengi ambayo hajajitokeza katika usemi wake. Mama alipotumia methali hii alikuwa akimuonya Tenge. Tenge tayari alikuwa ameshapata ujauzito na kumzaa mtoto jambo ambalo lilimfanya kukatiza masomo yake. Kwa kuwa alikuwa analielewa jambo hilo na tendo hilo, alikuwa hana budi kuepukana nalo. Haya yametokana na kauli kwamba

Tenge huenda akapata mchumba mwingine. Hivyo mama alikuwa akitoa onyo asije akadanganyika kama ilivyokuwa hapo awali.

### 2.4 Matumizi ya Tashbihi

Tashbihi hutokana na neno la Kiswahili 'shabihi' linalomaanisha kufanana, kulingana na kuwa sawasawa. Vitu viwili hulinganishwa kwa njia ya waziwazi kwa kutumia viungo kama vile " mfano wa '*kama*" *mithili ya*" "*ja*" na kadhalika.

(Kuhenga, (1977), Wamitila, (2003). Tashbihi hutumika kusisitiza kauli na kuepuka maelezo mengi. Katika tashbihi ni leksika moja tu ambayo huleta maana ya tashbihi hiyo. Hivyo basi kulingana na kanuni za utaratibu wa ushirikiano za Grice, utapata kuwa itakuwa vigumu kuzizingatia. Kwa mfano uchache wa maneno katika tashbihi yenyewe inakiuka kanuni ya idadi. Hii ni kumaanisha kuwa msikilizaji atapata changamoto kupata maana ya msemaji kwa kuwa maana katika upana na urefu wa tashbihi hiyo lazima ichunguzwe vizuri ili ilete maana lengwa. Kanuni ya ukweli pia hukiukwa kutokana na jinsi tashbihi hizo husemwa, humuacha msikilizaji akiwa na utata wa jinsi ya kupata maana iliyokusidiwa. Katika tashbihi maana huwa imebebwa tu na leksika moja. Leksika hiyo ikiwa ni nomino ya mnyama basi tabia za mnyama huyo ndizo zitakazotumika kubainisha maana ya tashbihi hiyo.

Katika *Mama ee*, Mwachofi ametumia tashbihi ili tupate alichomaanisha, hatuna budi kuchunguza undani wa maana ya tashbihi hizo na kutambua ni leksika zipi zinazobeba maana na zinaleta maana gani katika tamthilia ya *Mama ee*. Tunabainisha tamthilia hizo zilizosemwa na nani katika tamthilia na zilimaanisha nini kwa mfano.

> Mwavita: mtoto ameshikwa na homa kali. Mchana kutwa nimezurura kutafuta waganga na waganguzi sina wa kunisaidia,ni kama niliyefiliwa na mume au niliyezaa nje ya ndoa-ilhali jiume lenyewe levi lazururra na mgongo wa gari likibadilisha wasichana kama mashati. (uk 1)

Katika tashbihi ya kwanza leksika ambazo zimebeba maana ni kufiliwa na mume, na zaa nje ya ndoa. Kutokana na maneno haya tunatambua kuwa mke aliyefiliwa na mume huwa amezingirwa na upweke kwa sababu hana wakumliwaza. Pia katika utamaduni wa kiafrika ilikuwa vibaya

sana msichana au mwanamke kuzaa nje ya ndoa. Iwapo angefanya hivyo, basi angetengwa na kuwachwa katika upweke. Wakati Mwavita anaposema haya tunapata ukweli kuwa ingawa yuko katika ndoa, ndoa yenyewe imejaa upweke. Upweke huu unatokana na mumewe Kinaya ambaye anaonekana kutopata nafasi ya kushirikiana na kuleta amani katika ndoa yake. Kinaya amemwacha mkewe nyumbani huku akisononeka katika upweke. Katika tashbihi ya pili maneno ambayo yataleta umaanisho ni badilisha na mashati. Hivyo basi utapata ni muhali kupata mtu akiwa na shati moja kwenye mwili wake. Lazima awe nayo mengi ya kubadilisha. Hii ndio maana ya Mwavita kusema kuwa mumewe anabadilisha wasichana kama mashati. Alimaanisha kuwa Kinaya si wa mwanamke mmoja bali wengi ambao anawabadilisha kila wakati. Hivyo basi Kinaya ana macho ya nje. Kubadilisha kwake kwa wanawake wengi kunalinganishwa na jinsi mtu abadilishavyo mashati. Katika kusema hivyo basi kanuni ya ukweli ikawa imevunjwa.

> Kinaya: (*Akilalamika*) jike gani hili nililoowa! Kunifungulia mlango taabu na Hata niingiapo anitazama kama niliyetapakaa mavi! Nilichobeba hatizami. (uk 3)

Ukweli umekiukwa katika tashbihi hii kwa sababu kuna maana fiche. Katika tashbihi hii kuna maneno ambayo hayatoi maana ya waziwazi ya tashbihi hii. Maneno haya ni tapakaa mavi. Ikiwa mtu ametapakaa mavi basi atakuwa ananuka. Hivyo basi ikiwa atapita karibu na watu akiwa na harufu hiyo basi watamtazama kwa dharau na dhiki. Kwa sababu watakuwa wamekerwa zaidi. Kinaya alipotumia tashbihi hiyo alimaanisha kuwa mkewe ambaye ni Mwavita anamdharau sana na kumwona kuwa hafai. Hivyo basi anamaanisha kuwa Mwavita hamheshimu ilhali yeye ndiye kichwa cha familia hiyo.

> Mwavita: Ukitaja ya Tenge wanilazimu kukuelezea ya dada zako. Dada zako wako wote, wako wapi? wazurura ovyo mjini kama mbwa koko bila mabwa. (uk 10)

Leksika ambazo zinafaa kuchambuliwa ili tupate maana lengwa ni zurura na mbwakoko. Mtu anapotembea lazima awe na kule anakoenda. Mbwakoko wamejulikana kwa kuzurura kwao bila sababu na kutokuwa na kwa kukaa au kwa kwenda. Ukweli hapa umekiukwa kwa sababu Mwavita aliposema hivyo alikuwa akimnyamazisha Kinaya ambaye alikuwa amemkera kwa

kumwambia kuwa Tenge hana pa kwenda. Hivyo alikuwa akimaanisha kuwa dada zake Kinaya pia hao hawana waume na wamebaki tu kuzururazurura wasijue waendako na watokako na hawana sababu ya kuzurura kwao. Kanuni ya nama pia ilikiukwa kwa sababu ikiwa Mwavita angemuelezea Kinaya ukweli mambo basi huenda kungezuka vurugu ambayo ingekatiza mawasiliano.

> Mama: Una nini mwanangu? Mbona waomba kama uliyefiliwa?

Katika tashbihi hii kuna maneno ambayo yameficha maana halisi ya tashbihi yenyewe. Maneno yenyewe ni omba na filiwa._ Mtu ambaye amefiliwa huwa amefikiwa na machungu. Kwa hivyo anapolia huwa anawaomba wenzake kwa yale machungu anayopitia. Hivyo basi watu humuonea huruma. Tenge alipofukuzwa shuleni, ndipo alipogundua kuwa yaliyomngojea yalikuwa mazito. Aliona kuwa amekosea wazazi wake sana hivyo basi akawa anamuomba mama yake amsamehe. Kwa vile mama yake hakuelewa kilichokuwa kinaendelea basi akawa anashangaa jinsi vile Tenge alikuwa akimlilia hadi kumfananisha na mtu aliyefiliwa.

> Mama Mwavita: Mwavita basi mama Utalia kama uliyeambiwa amkufa? basi mama(uk 37)

Watu hulia sana wanapompoteza mmoja wao, au wanapoarifiwa kuwa mmoja wao amewaaga. Wao hulia sana kawa kukosa matumaini ya kumwona tena mpendwa wao. Mwavita alikuwa akimlilia mtoto wake ambaye alikuwa amebaki na baba yake, yaani Kinaya. Alikuwa amemkosa mwanawe kwa muda. Hii ndio sababu ya mamake kumliwaza kwa kumwambia kuwa mtoto wake angali hai hivyo basi pana matumaini makubwa ya wao kutangamana na kuweza kuwa pamoja.

> Mwavita: Je, ukiishi bila kuona haya na kusemwa na kutiwa aibu, lakini huna raha maisha yako yanapita kama jinamizi, siku zote uko jahanamu faida gani unapata? Heshima! Ndiyo watu watakuheshimu. Lakini…….(60)

Maneno ambayo yana maana fiche katika tashbihi hii ni jinamizi. Jinamizi ni ndoto ya kutisha. Ni ndoto ambayo humfanya mtu agutuke usingizini na kuwachwa akiwa katika hali ya kushtuka.

Mwavita alipotumia tashbihi hii alikuwa aikimaanisha kuwa ndoa yake imekosa raha kabisa. Anaona afadhali ukweli usemwe kuwa heri kumzaa mtoto haramu kuliko kuwa katika ndoa ambayo haikupi raha wala amani. Hivyo basi anaona kuwa ndoa yake ni ya matatizo chungu nzima. Imejaa vita, matusi na ni ya kumfanya kujutia kuolewa. Kanuni ya namna imekiukwa kwa sababu kuna utata katika kubaini alichokuwa akimaanisha. Kanuni ya ukweli imekiukwa. Ukweli katika tashbihi hii umefichika na unahitaji uchambuzi wa kina.

> Mwavita: Si huyu shemegi yako! Mtu anuka kama mtungi wa tembo. Ondoka hapa wanizidishia maradhi.(uk 64)

Katika kusema haya "mtu anuka kama mtungi wa tembo" kanuni ya namna imekiukwa. Kwa sababu Mwavita hakutaka kusema waziwazi kuwa Kinaya alikuwa akinuma pombe kwa vile alikuwa amekesha ulevini.

> Mwavita: Wajua mama wake wataendelea kunyonywa na kunyanyaswa na mabwana kwa kutojua haki zao. Wengi washakubali kuwa wananchi wa tabaka la chini! Ati ndivyo Mungu alivyotuumba. Wake kama hao huwachukua waume kama miungu.(uk77)

Miungu kwa wale walioiabudu waliichukulia kuwa ya dhamana. Waliweza kuiabudu, kuiheshimu hata kuitii huku wakihofia adhabu yao wakati wa kuikosea. Waume kuchuliwa kuwa kama miungu katika tashbihi hii ina maana kuwa wanawake wamebaki kuwaogopa, kuwatii kupita kiasi, na hata huenda wakawa wanawaabudu. Hivyo ni kumaanisha hamna chochote watafanya pasi na wao waume kunena. Ndipo Mwavita analamikia wake wa aina hiyo akiwaona kuwa ndio wanaokandamiza uhuru wa mwanamke. Katika tashbihi ya pili neno sumu ndilo limebeba maana ya msemaji. Sumu ni kitu chochote ambacho anapokila binadamu au kiumbe chochote chenye uhai, uhai huo hukatizwa au huenda sumu hiyo ikalatea madhara makubwa katika viuongo vya mwili wake. Mama anapotumia tashbihi hiyo, anamshawishi mwanawe Mwavita ambaye anapitia machungu ya ndoa kuwa asiwe wa kuweka maneno ya kuumiza roho yake. Awe ni wa kuyasema yale ambayo yamejaa moyoni. Anapomwambia hivyo anamaanisha kuwa kuna maneno mengine ambayo huwa ni machungu zaidi na ya kuweza kuumiza roho ya mtu bure.

Mwavita: Najiona kama niliyegutuka ndotoni. Yale niliyodhania kuwa kweli sio kweli kabisa.(uk 90)

Mtu akiwa usingizini huwa anaota. Ndoto zingine huwa nzuri na zingine mbaya na za kutisha. Vilevile katika mawazo ya mtu huwa anaazimia kufanya jambo fulani kupata kitu fulani au hata kuwa na maisha ya aina fulani. Hizo zote ni ndoto. Wakati mwingine ndoto hizo hutimia na wakati mwingine hukosa kutimia. Wakati Mwavita aliolewa, alifikiria kuwa ndoa ndiyo mwanzo wa mambo mazuri duniani. Hakutarajia ayapitie yaliyokuwa yakimkumba. Alipojua ukweli wa mambo kuhusu ndoa, alijioma kuwa ni kama alikuwa akilala kisha akizinduka usingizini na kupata ukweli wa mambo kuwa kumbe ndoa ndicho chanzo cha matatizo ya jinsia ya kike ulimwenguni. Ni kutokana nay ale amesema tunapata kuwa kanuni ya namna imekiukwa. Kuna utata katika kupata ukweli wa mambo.

## 2.6 Matumizi ya Majazi

Mtu au mahali hujulikana kutokana na sifa zake, tabia, hulka au hata mienendo yao. Badala ya msanii kutolea maelezo hayo kuhusu mtu yule au mahali pale, atatafutia jina linaloambatana na tabia, hulka, mienendo na sifa zake ili kuweza kumfanya msomaji au msikilizaji kupata maelezo zaidi kuhusu mtu yule. Jina hilo atakalompa mtu yule au mahali pale basi ndilo litakuwa limetumika kama majazi. Mbinu hii humfaidi msomaji au msikilizaji kuupata ujumbe fulani, kuwa na mwongozo kuhusu yaliyozungumziwa kuhusu mahali pale au mtu yule. Kwa kuwa majazi ni jina moja tu ambalo limebeba maelezo mengi kuhusu mhusika fulani, hivyo basi utapata ni kanuni ya idadi na ukweli katika utaratibu wa ushirikiano, kulingana na Grice ambazo huvunjwa na kuleta umaanisho. Katika *Mama ee*, mwandishi ameweza kutumia mbinu hii na hivyo kumfanya msomaji kuweza kuelewa zaidi kuhusu wahusika hao. Kwa mfano kuna mhusika mkuu wa kike ambaye jina lake ni Mwavita. Katika kufanya uchunguzi wa ndani jina hili huenda limeundwa kutokana na majina mawili. Kwa mfano mwanamke mwenye vita , tukipata ufupisho wake Mwavita au ni mwana aliye na vita pia tukapa ufupisho wake Mwavita. Je, huyu Mwavita ana sifa za vita au la? Kwanza kabisa mwanzoni mwa mchezo, tunamuona akimzomea mumewe anapoingia akiwa mlevi chakari. Anaonekana kumzomea kwa kumrushiwa cheche za manene makali. Hapo ikadhihirika kuwa kweli yeye ni mwenye vita vya maneno.

Tunapofikia sura ya mwisho ya mchezo huu tunapata kwamba wakati Kinaya alikuwa amewatembelea Mwavita na Tenge baada ya kuwachana kirasmi katika korti, alikipata cha mtemakuni pale ambapo Mwavita na dada yake walipomvamia na kumpa kichapo cha mbwa. Licha yake Mwavita kuwa mwenye vita vya maneno pia yeye ni mwenye vita vya kimwili. Alipigana sawasawa. Mwisho katika hali yake ya kupigania uhuru wa jinsia ya kike, hapo ndipo jina lake linaenda sambamba na tabia, mienendo, hulka na sifa zake. Yeye ni mpiganiaji wa uhuru wa jinsi ya kike katika dunia ya ubabedume.

Mhusika wa pili ni Kinaya. Pia yeye ni mhusika mkuu katika tamthilia hii. Kinaya maana yake kulingana na Maitaria (2014) ni mbinu ambayo hutumiwa na mwandishi ili kuonyesha kinyume cha matarajio. Ni namna ya kutoa kauli ambayo inasimama kinyume au ukweli ulivyo. Wakati Mwachofi alimpa mhusika huyu wa kiume jina Kinaya, je alimaanisha kuwa yuko kinyume cha matarajio ya waume katika jamii? Jibu la swali hili ni ndio. Kama ilivyokawaida, mume katika jamii ndiye husimamia majukumu na matakwa ya wanajamii wake. Mume ndiye huhakikisha watoto wamekula, wamesoma, amelipia kodi na kumtunza mke wake. Kinyume na alivyo Kinaya ambaye majukumu haya yote amemtwika mkewe ilhali yeye yuaonekana tu baba wa kuguruma katika nyumba ile bila matendo yoyote. Hapo ndipo jina lake linaenda sambamba na tabia zake. Yeye anafikiria kuwa ukiwa mke na umlipie mahari basi ameshakuwa mali yake na unaweza mtumia jinsi utakavyo. Haya yote si ya kweli na hivyo kuonekana kuwa yeye “si mume” akilinganishwa na wa zama za mababu zetu.

Tenge pia ni mhusika aliyepewa jina la Kimajazi. Tenge maana yake ni mambo kwenda mrama, ghasia au fujo. Tenge katika tamthilia hii ni mtoto wa kike ambaye tunaona kuwa kitumbua chake kikiingi mchangani wakati ambapo alipata ujauzito akiwa angali shuleni. Mambo yake yalikwenda mrama kwa sababu alikuwa hana budi kuwacha shule. Ikiwa alikuwa na ndoto yake katika maisha baada ya kumaliza chuo, basi ndoto hiyo haikuwa tena. Yeye ni wa fujo kweli. Kwa mfano alipokutana na aliyekuwa baba wa mtoto wake. Katika hali hiyo tunamuona akizusha fujo pale ambapo alimwambia kuwa mtoto yule si wake. Aliweza kumtetesha kwa cheche za matusi hadi akasababisha watu kufurika mahali pale ili waweze kushuhudia kilichokuwa kikitendeka. Aliweza pia kuzusha fujo huku akimsaidia Mwavita dada yake kwa kumpiga Kinaya. Ni kutokana na sifa hizo tunapata kuwa alipewa jina sawa na tabia zake.

### 2.7 Misemo na Nahau

Misemo ni mafungu ya maneno ambayo hutumika na watu wa jamii fulani ili kukuza maadili, kuelimisha na hata kuonya. Nahau ni mbinu ya kutumia maneno ya kawaida ilhali maneno hayo hutoa maana tofauti na ile iliyo kwenye maneno ambayo yaliyotumika. Ijapokuwa nahau hutumia maneno ya kawaida, kauli yake huwa na undani kiasi kwamba lazima msomaji au msikilizaji awe makini kupata tafsiri bora ya nahau hiyo. Kwa vile misemo na nahau hazina maana ya moja kwa moja, huzua umaanisho. Umaanisho huo hutokea kwa kuwa idadi ya maneno, yaliyotumika huwa ni chache hivyo kumfanya msomaji au msikilizaji kutatizika katika kupata alicholenga mwandishi au msemaji. Kanuni ya ukweli pia hukiukwa kwa sababu hutachukulia nahau au msemo ule jinsi ilivyo. Lazima uweza kufanya utafiti wa ndani ili kupata fasiri bora. Kanuni ya namna pia hukiukwa sawa pale ambapo anayetumia misemo au nahau, huitumia kwa njia tata yakumfanya msikilizaji au msomaji wa kauli ile kutopata maana lengwa kwa njia ya moja kwa moja. Katika kufanya hivyo misemo na nahau huzua umaanisho aidha katika mazungumzo au katika kazi yoyote ya fasihi andishi au simulizi.

Kwa mfano katika *Mama ee* misemo na nahau imetumika kwa wingi. Imesaidia katika ujenzi wa maudhui ya tamtiilia hiyo. Mifano ni kama vile.

> Mama: Nisikize nini? Ungekuwa ukinisikiza <u>bila komango</u> masikioni haya <u>hayange jitokeza</u>.(uk 14)

Mtu anapoambiwa kuwa ametia Komango masikioni, haimanishi kuwa alichukua komango kisha akaziweka ndani ya masikio yake. Neno “Komango na masikio” ndiyo yamebeba maana ya ndani ambayo ni ya msemaji. Mtu akitia Komango anamaanisha hatakuwa na uwezo mzuri wa kusikia. Mama anapotumia msemo huu anamaanisha kuwa ikiwa Tenge angemsikiza bila kupuuza aliyokuwa ameambiwa, asingepatwa na msiba ule wa kupata mimba akiwa angalia shuleni. Hivyo basi inamaanisha Tenge alikuwa wa kupuuza wosia aliopewa na wakubwa wake.

> Baba: Kila siku. George amekuja! George amekuja kumbe ndiyo hayo umepata. natija sasa! George yuko shuleni! Wewe je? <u>Umeambulia patupu.</u>(uk 15)

Kuambulia patupu ni kukosa ulichotumainia au kushindwa kupata ulichotarajia. Wakati baba alitumia msemo huu alikuwa akimaanisha kuwa Tenge hataweza kupata alichotarajia katika

masomo yake kwa sababu alikuwa amefukuzwa kwa sababu ya ujauzito hivyo kukatiza masomo yake. Kanuni ya idadi imekiukwa, kwa sababu ambulia patupu ni maneno mawili tu ambayo yamebeba maana iliyo pana.

> Kaka: Baba tafadhali usimpige mama lakini hili sichana lako litanitambua hizi nguo zote nendazitie moto maana ndizo zilizomfurisha kichwa ati ni nzuri.(uk 16)

Katika msemo huu "kufuriha kichwa" hakuna vile utachukulia maana ya juu kwa kuzingatia maneno yaliyotumika. Kwa mfano hutasema kuwa kufura kichwa ni hali ya kichwa kuvimba na kupata umbo la ukubwa. Kaka yake Tenge alipotumia msemo huu alikuwa akimaanisha kuwa Tenge alikuwa na kiburi sana asiweze kuambilika na kilichompa kiburi ni nguo zake alizoziona kuwa za kupendeza mno, ndipo alitaka kuzichoma. Kanuni ya ukweli imekiukwa kwa sababu maneno "fura kichwa" yana maana ya ndani yaliyobeba ukweli.

> Mzee wa kijiji: mwanangu hapo unaanza <u>kuvuka mpaka</u>. Usizidishe mambo tunayotaka kuyapunguza.(uk 29)

Maneno kuvuka mpaka_ ndiyo yamebeba maana ya msemaji katika msemo huu. Ikiwa utachukulia maana ya kawaida ya maneno haya, basi hutaweza kupata maana ya masemaji. Mzee wa kijiji alikuwa akimpa onyo Ba mkubwa Mwavita kwa sababu alionelea kuwa alikuwa amezidi sana na kuonekana kuongea maneno mengi yaliyokuwa machungu sana kuhusu ndoa ya Kinaya na Mwavita na hiyo akawa amepita kiasi ya yale yaliyokuwa yakizungumziwa. Kanuni ya namna imekiukwa ili kusiwe ba kutoelewana ambako huenda kukakatiza mawasiliano.

> Ba mkubwa Mwavita: Aliyosema mwenzetu tumekubali. Kosa lazima <u>liwe na fimbo</u> yake, lakini unapomwadhibu mtoto huwi wamuua.(uk 33)

Kanuni ya ukweli imefichika kwa kutumia neno fimbo kumaanisha adhabu.Msemo huu ulitumika wakati Kinaya alikuwa amechunguzwa na kutokana na maelezo ya Mwavita, ilionekana kuwa alikuwa ametenda makosa hayo. Ni kutokana na hayo alikuwa hana budi kukabiliwa adhabu yake. Msemo huu ulikuwa unamaanisha kuwa kila kosa lina adhabu yake.

Hivyo basi neno fimbo katika msemo huo ukawa na maana ya ndani ya adhabu. Adhabu hiyo ilikuwa faini ambayo Kinaya angetozwa kutokana nayale aliyotenda.

Mzee wa kijiji: Eleza yote mke wangu. Usiba`kishe kitu kikakukera moyoni. Leo ni siku ya kufua moyo usibaki na undani wowote na mtu yeyote.(uk 38)

Maneno “Kufua na moyo” yamebeba maana ya msemaji katika msemo huu. Kwa hivyo ikiwa utachukulia maana asili ya maneno haya na ukafafanua msemo huu basi hutaweza kuafikia maana ya ndani aliyokuwa akimaanisha msemaji. Kwa mfano ikiwa utatoa maana kuwa kufua moyo ni kuchukua maji na sabuni pamoja na karai ukaanza kuusafisha moyo utakuwa umekosea. Tunaelewa kuwa mtu akiwa na mambo mengi moyoni huwa yanamkera na hivyo kuonekana kumletea uchafuzi moyoni. Mzee wa kijiji alikuwa akimshauri Mwavita aweze kuyaeleza yote bila kuficha aliyokuwa akipitia katika ndoa yake. Aliendelea kumwambia ayatoe yote ili lisibaki hata moja la kuendelea kumletea huzuni. Hivyo basi kufua moyo ni kuyasema na kuyatoa yote yaliyo moyoni ambayo yanakukera na kubaki na moyo safi. Ni kukiri yote bila kubakisha.

Katika msemo wa pili mzee wa kijiji aliposema kuwa hakuna mtu wa mbali, alikuwa anataka Mwavita kuyasema yote bila kuogopa kwa sababu hakukuwa na yeyote wa kutoa siri au maneno haya kwa kumwaga mtama mbele ya kuku wengi. Hii ina maana kuwa watu wa mbali ni wale wa kutoa siri na ambao huenda hawawa takii mazuri. Haina maana na mtu wa kutoka masafa marefu na kwenu. Katika misemo hiyo kanuni ya namna ikawa imekiukwa.

Mwavita: Hayaachi hayo! Mimi niliingia kivulini kweli kweli! Sijui ni nani aliyetunga sheria ya watu kuoana.(uk 59)

Mwavita alikuwa akijutia kufanya uamuzi wake kurudi kwa Kinaya kabla hajatimiza matakwa ya watu wa upande wa akina Mwavita. Alipomrudia alifikiri kuwa huenda akabadili tabia zake. La mno lilimfanya arudi ni mtoto wake Juma. Lakini mambo yalikuwa mabaya hata kuliko mwanzo. Hivyo Mwavita aliposema kuwa yeye aliingia kivulini, hakumaanisha kuwa alikuwa chini ya mti wakati wa jua kali. Bali alimaanisha kuwa alikuwa katika lindi la taabu na dhiki. Katika kusema hivyo akawa amekiuka kanuni ya namna.

Mama*:* Chai hiyo itaingia wapi! Huzuni imenikaba roho.Mambo yamenitumbukia nyongo kumwona Mwavita katika hali hii.(uk 75)

Baada ya Mwavita kuonelea kuwa awachane kabisa na mambo kuhusu ndoa yake, aliweza kuamua kujitenga na akapata nyumba ambayo aliishi pamoja na dada yake. Mama yao kusikia hivyo basi aliweza kupanga kufunga safari ili awatembelee. Mama alidhani kuwa kwa vile wamejitenga basi wameweza kupata raha zao. Kinyume na hayo, mama alipokuja alimpata Mwavita akiwa katika hali ya kusononeka, huzuni tele na bila raha yoyote. Ndipo mama akaona ni kama vile matarajio yake yalikuwa kinyume na jinsi hali ilivyokuwa. Ndipo aliweza kutumia msemo huo. Alimaanisha kuwa kinyume na matarajio yake, bado watoto wake walikuwa hawajapata raha. Ili asionekane kumlaumu Mwavita kwa kutosimama imara kwa uamuzi wake, basi kanuni ya namna ikakiukwa.

Mwavita: Nikisema moyo wangu waanza <u>kuwa mwepesi.</u> Naona kama naanza <u>kutua machungu..</u>(uk 78)

Wakati huu Mwavita alikuwa ameyasema yale yaliyokuwa yakimkera moyoni. Huu ni wakati wa kuongea kwake na mama na dadake Tenge. Hapo aliweza kuona kuwa ameweza kuyatoa yote. Mambo hayo yalikuwa kama mzigo mzito mabegani pake. Aliposema kuwa ameanza kutua machungu, haimaanishi kuwa alikuwa ameyabeba kwenye mzigo aliojitwika kichwani au mabegani. Kanuni inayovunjwa hapa ni ya ukweli. Alimaanisha kuwa kwa kuyasema tu yalikuwa yamemwondokea na kumwacha akiwa mwepesi. Bila kuwa na ya kumfinya moyoni mwake.

Mwavita: Po wakufuru! <u>Tema mate!</u> Waombe nyanya zako wakusamehe kwa hayo uliyotamka.(uk 89)

Maana asili ya maneno haya “tema mate” hayawezi kutumika kuleta maana ya nahau hii. Kuna kile kitendo cha kutema mate kutoka mdomoni. Ikiwa utachukulia hiyo kuwa maana ya nahau hii basi utakuwa hujalenga maana ya msemaji. Mwavita alikuwa akijutia kuzaa na Kinaya mtoto kwa sababu alikuwa haishi tena na mumewe na mtoto huyo. Katika kujutia kwake ndipo mama akamkemea kwa kumwambia ateme mate na hata kuwaomba nyanya zake msamaha. Mama

alikuwa ameshangazwa sana na jambo hilo la Mwavita kufikiri kuwa heri kuishi bila kuzaa mtoto. Basi akamwonya kwa msemo huu unaomaanisha kuwa Mwavita azike fikira hizo katika kaburi la sahau na asiweze kufikiri au kusema vile tena. Mama aliweza kukiuka kanuni ya namna.

> Mama: Simama hapo mbele yangu nijue mbivu na mbichi, maana nasikia kuna jambazi utembealo nalo siku hizi. Simama!(uk 92)

Mama amevunja kanuni ya namna. Kutokana na aliyoyasema ‘mbivu na mbichi’ ni wazi kuwa kuna kile ambacho anachunguza lakini hakisemi kwa njia iliyo wazi. Mama alipowatembelea wasichana wake alikuwa na mengi sana. Haikuwa tu kuwajulia hali bali kuweza kupata ukweli bayana kuhusu yale yaliyokuwa yakizungumziwa kuhusu Tenge. Mtu akitaka kujua mbivu na mbichi haimaanishi kuwa kuna pengine matunda ambayo anataka kuchagua yaliyo mabivu na mabichi. Mama aliposema sema hayo alikuwa akimaanisha kuwa anataka kujionea na kusikia mwenyewe yaliyo ya ukweli kuhusu Tenge. Alipomwambia asimame alitaka kujua ikiwa ni ukweli kwamba alikuwa mjamzito kutokana na zile fununu alizozipata kule nyumbani. Kwa hivyo alitaka kujua kila kitu, ukweli wote na undani wote wa mambo hayo, bila kuegemea yale aliyokuwa amesikia.

Kuna kile kitendo cha kuongeza chumvi pengine katika chakula ili kiwe na ladha tamu. Hii siyo maana inayojitokeza katika msemo huu. Tenge alikuwa amekutana na George aliyempachika mimba na kumkana. George ndiye aliyefanya Tenge kuwacha shule. Walipokutana Tenge alikuwa amempata katika hali ya kutatanisha. Hii ni kwa sababu kutokana na maelezo yake, George alikuwa ni kama mambo yalikuwa magumu kwake. Katika maelezo hayo Tenge alionekana kusema yasiyokuwa ya ukweli kulingana na Mwavita. Ndipo Mwavita akataka kujua ikiwa Tenge alikuwa anasema ya ukweli au alikuwa akiongezea porojo. Hivyo basi kuongeza chumvi ni kudanganya au kusema mengi yaliyojaa porojo nyingi. Mwavita hakuamini yale Tenge alisema alifikiri alikuwa akidanganya au ni maneno yenye porojo nyingi. Badala ya Mwavita kumwambia Tenge aeleze yaliyo ya ukweli na asiwe anadanganya, hapo kanuni ya namna ikakiukwa.

## 2.8 Matumizi ya Mbinu Rejeshi

Mbinu rejeshi hutumiwa wakati wa kurejelea yale amb**ayo** yalitokea hapo awali kwa mujibu wa kuleta maana fulani unapoyaunganisha na yanayoendelea wakati huo. Mbinu rejeshi huleta umaanisho kwa sababu yale ambayo yanarejelewa huwa hayana uhusiano na yale yanayozungumziwa kwa wakati ule. Wakati mwandishi anapotumia mbinu hii, huwa anataka kuleta uwiano wa yale ya awali na yale ya kisasa. Hivyo basi atakuwa anataka msomaji au msikilizaji kuleta aweze kupata kuoanisha matukio hayo mawili na kupata fasiri bora ya aliyomaanisha. Kwa mfano katika *Mama ee.*

> Nyanya: Zamani zetu sisi sheria zilikuwa zafuatwa sana. Kamwe haikuwezekana mtu kuwa mlevi na kwenda kwa mkwewe. Hata mkwe akiwa na sherehe na kuwa na tembo, babamkwe atalewa lakini mtoto kamwe halewi. Huwekewa tembo lake kando aende lewa baadaye lakini siyo mbele ya wakweze.(uk 30)

Maneno yake nyanya hayendi sambamba na yale yanayozungumziwa kwa wakati huo. Nyanya alikiuka kanuni ya uhusiano. Katika kufanya hivyo alitaka Kinaya aweze kuzitambua sheria na utamaduni ili wakati mwingine asije akwakosa tena**.** Nyanya alipokuwa akitoa maelezo haya alikuwa akimrejelea Kinaya ambaye inasemekana kuwa alikuwa amewakosea wakwe zake wakati wa kwanza alipomkosea Mwavita na akawa amekuja kuwaomba msamaha. Wakati huo Kinaya alionyesha madharau kwa kuja huku amelewa na pia hakuongea kwa njia ya heshima. Kwa hivyo alichomaanisha nyanya ni kuwa Kinaya hakuwa na heshima hivyo akawa anataka ajirekebishe wakati huu wa pili kutaka kupatanishwa tena na Mwavita. Kisengere nyuma hicho kwa ufupi ni cha kumtaka Kinaya atambue sheria na utamaduni ili aweze kutangamana vizrui na watu wa ukoo huo.

## 2.9 Matumizi ya Kejeli

Kejeli ni ile hali ya kutamka maneno ambayo huwa yanaumiza sana msikilizaji au msomaji yanaposemwa, yanapozungumzwa na hata yanapoandikwa. Kejeli ni aina ya mbinu ambayo hutumiwa kwa kusudi la kumgusa mtu kwa njia ya waziwazi ambapo mara nyingi ni kwa sababu ya kuweka wazi au kufichwa ubaya au udhaifu fulani alionao mhusika fulani. Kwa mfano;

Kaka: Nyamaza wewe. Walilia nini? Si umepata ulichotaka? Kupoteza pesa eti wasoma! shahada uliyopata ni kubwa kweli kweli!(uk 17)

Haya ni maneno yalisemwa na kakake Tenge. Alikuwa akimkejeli Tenge kuwa alikuwa akijidai kuwa anasoma. Kwa kumwambia kuwa sasa alikuwa amepata shahada kubwa kweli kweli, si ukweli. Hii ni kwa sababu tayari alikuwa mjamzito akiwa bado hajakamilisha kidato cha nne. Ukweli ni kuwa kakake Tenge alikuwa anamaanisha kuwa Tenge hakuwa msomi kabisa. Alikuwa amepotelea katika raha na hivyo akawa amepata zawadi yake. Hapo basi kanuni ya ukweli ikawa imekiukwa.

Mzee wa kijiji: Yule mtoto kamfunzeni juu ya kuishi na bwanake msiketi naye bure.(uk 57)

Nyanya: Basi kazi yangu imekuwa leo unifunze wewe? Njoo kamfunze basi!(uk 39)

Mzee wa kijiji kwa kusema hivyo anamaanisha kuwa ni jukumu la kina mama kufunza Mwavita mambo ya ndoa. Naye nyanya kwa utani anamaanisha kuwa wao kama kina mama tayari wanatambua jukumu lao kwa Mwavita. Hamna haja ya kuambiwa na kukumbushwa. Pia tunaona kanuni ya namna ikikiukwa.

Mwavita: Kwa ajili ya kupiga pasi tu! Nguo hizo ni za sherehe ya wevi au ni za kuenda katika ufalme wa mbingu ya saba.(67)

Kinaya: ukiambiwa ufanye kitu mgonjwa, kukitokea kondo si mwele tena u tayari kupigana.(uk 67)

Wahusika hawa wamekiuka kanuni ya namna na ukweli. Jinsi ambavyo wameyasema maneno hayo kuna utata hivyo basi kumfanya mtu kutoelewa haraka yanayosemwa. Kanuni pia ya ukweli imekiukwa. Mwavita anamaanisha kuwa mwanamke daima adhalilishwa hata kwa majukumu madogomadogo ambayo hayajayatekeleza. Kwa sababu anaona kuwa Kinaya hana haja kujua walivyo bali anaingia kwa fujo huku akitaka kufanyiwa kila kitu. Kinaya naye kwa upande wake anamaanisha kuwa Mwavita hatekelezi wajibu wake kama mke nyumbani huku

akisingizia ugonjwa. Hamuoni kuwa ni mgonjwa. Kwake ni kama mzaha. Hivyo kudunisha wanawake.

## 2.10 Matumizi ya Maswali ya Balagha

Haya ni maswali ambayo msemaji huwa anauliza lakini hayahitaji majibu yoyote. Kutokana na maswali haya msomaji au msikilizaji huwa anapata maana ya ndani au yale yaliyolengwa na msemaji. Kwa mfano.

> Kinaya: *(Nje)* We mwanamke fungua mlango haraka. Wasema na nani huko Ee?kwani hukusikia gari langu au lazima nibishe ndipo nifunguliwe? (uk 2)

Kinaya alikuwa amekasirika sana kwa sababu ya mke wake kuchukua muda mrefu kabla ya kumfungulia mlango. Ina maana kuwa anaona kama Mwavita hatekelezi majukumu yake kama mke. Hivyo akawa amekasirika. Amemeweza kuvunja kanuni ya namna kwa sababu ametumia swali ambalo limebeba maana ya ndani.

> Mama: Tangu lini wanawake wakapigwa kwa ngumi? Huyo mume alikosa wanaume wa kupigana nao? Na wewe utalipiwa na nani sasa? Wapendwa je mbona ngumi sasa?(uk 13)

Mama alalamika mateso ya msichana wake Mwavita ambaye anaonekana kupitia katika mateso ya ndoa kwa kupigwa. Bado mama hajagundua kuwa Tenge ni mjamzito. Anaposema kuwa *"na wewe karo utalipiwa na nani sasa?"*Anamaanisha kuwa wakati Mwavita na Kinaya wanavurugana, hakuna vile Tenge atalipiwa karo hivyo masomo yake yatakatizwa. Hivyo kanuni ya namna inakiukwa ili kuleta maana ile.

> Mama: Mabibi na mababu zangu mlionitangulia! Nimekosa nini kikubwa sana hata yote haya yanipate mimi?(14)

Mama anajutia yale ambayo anakumbana nayo kwa sasa. Kwanza kabisa ni kuteswa kwa Mwavita kwa kupigwa katika ndoa yake. Pili ni kufukuzwa kwa Tenge shuleni baada ya kugunduliwa kuwa ni mjamzito. Haya yote yakawa juu yake mama. Hii ni kwa sababu lawama zote zitamwendea kwa kukisiwa kuwa hakuwafunza wanawe vizuri.

Baba: kosa la mara moja kwani hukujua mwisho wake? Huyo mamako hakuwaambia? umepata sasa! George yuko shuleni!weweje! kutokana na maswali haya kweli baba amekasirishwa sana na hali ya Tenge. Hataki kuambia kuwa lilikuwa kosa la mara moja. Ananyooshea mama kidole kwa kukosa kuwafunza wanawe. Katika kusema hivi kanuni ya ukweli imekikwa. Kwa sababu ni kutokana na maswali haya unafaa kuchambua kiundani ili kupata alicholenga msemaji.(uk 15)

Baba amekasirishwa sana na kitendo cha Tenge kupata ujauzito akiwa bado shuleni. Kanuni ya namna imekiukwa kwani anachomaanisha baba ni kuwa mama hakutimiza wajibu wake kuwalea watoto wake wasichana.

**2.11 Matumizi ya Kinaya**

Maitaria (2014) anafafanua kinaya kama mbinu ambayo hutumiwa na mwandishi ili kuonyesha kinyume cha matarajio. Hii ni hali ya kutoa kauli ambayo inazana na jinsi ukweli wa mambo ulivyo. Wakati kunaibuka Kinaya katika kazi yoyote ya fasihi, huwa kuna maana fiche, ambayo ni umaanisho. Umaanisho huu hujitokeza wakati kanuni mojawapo ya zile nne za utaratibu wa mawasiliano inapovunjwa. Kwa mfano katika *Mama ee.*

Padre: Sheria ya Mungu yasema tusameheane naye atatusamehe.Mimi kwa kufuata sheria hiyo ningemsamehe.(uk 85)

Padre hapa amejikanganya kweli, anaposema sheria ya Mungu inasema tusamehe ndipo yeye Mungu atusamehe, tunamuona Padre akiwa amemkataza Mwavita asishiriki komonio. Pia amekataa kumwekea mtoto wa Tenge wakfu kwa kusingizia kuwa ni mtoto haramu. Ikiwa kweli yeye amesimama kuwakilisha dini tunaona akifanya kinyume na matarajio. Kwa kufanya hivyo ameweza kukiuka kanuni ya namna kwani anayoyasema ni kusema tu kwa vile yameandikwa wala si kwa kuyatekeleza.

**2.12 Matumizi ya Chuku**

Wakati wa mazungumzo, ikiwa mtu anataka kusisitiza jambo fulani ili liweze kusawiriwa vizuri katika akili za msomaji au msikilizaji, basi yeye hutumia chuku. Chuku ni ile hali ya kuongesea

chumvi katika hali fulani. Pia ni hali ya kusema uongo katika kulifanya jambo lionekane la ukweli.

Kwa mfano katika *Mama ee* ;

> Kinaya: Basi huo ugonjwa umekuwa wimbo.Simama juu ya KICC uimbe kila mtu akusikie basi.(uk 7)

Kinaya alisema haya kutokana na vile Mwavita alikuwa amemkumbusha kuhusu magonjwa ya zinaa aliyokuwa amemwambukiza. Kinaya naye kwa kuburi chake anatia chumvi kwa kusema kuwa Mwavita aende akasimame juu ya KICC akaweze kutangazia kule. Kinaya ameweza kukiuka kanuni ya namna. Anavyosema basi ni wazi kuwa hajali kabisa hali ya mkewe.

> Mwavita: Mtu avumilie mpaka moyo umee sugu! Siwezi maana sugu hiyo nina hakika itapunguza utu wangu na hisia za kibinadamu, siwezi kuwa kama mashini ya kuzaa, kupika na kutoa raha wakati anapozihitaji mume.(uk 76,77)

Kwa kurejelea yale Mwavita alikuwa amepitia katika ndoa yake, yalikuwa ni makuu. Hapo ndipo Mwavita aliamua kujinasua na kupata uhuru wake. Kutokana nay ale amesema ni wazi kuwa alikuwa ameamua kutodhalilishwa na mume kwa sababu ya ndoa. Hivyo basi kanuni ya namna ikakiukwa

## 2.13 Hitimisho

Sura hii imedhihirisha kuwa umaanisho umejitokeza wakati wa kutumia matumizi mbalimbali ya lugha katika kuandika kazi ya fasihi ambayo ni tamthilia. Katika matumizi hayo ya lugha utapata kuwa ni leksika moja au mbili ambazo zinaibua umaanisho huo wa kukufanya ufanye uchambuzi wa ndani ili upate kuelewa alicholenga mwandishi au alichomaanisha mhusika katika kazi hii.

Tumeweza kuziteua na kubanini ni kwa jinsi gani umaanisho unaibuliwa kwa kurejelea tamthilia ya *Mama ee.* Kisengere nyuma huzua umaanisho kwa kukiuka kanuni ya uhusiano na namna ambayo unahitajika kufanya utafiti wa ndani kupata kilichomaanishwa. Maswali ya balagha, chuku na kejeli mara nyingi yanakiuka kanuni ya namna. Kwa hivyo kwa kutumia nadharia ya umaanisho tumeweza kuchambua matumizi ya lugha katika *Mama ee* na kubaini kilicholengwa.

# SURA YA TATU

## UKIUSHI WA KANUNI ZA UTARATIBU WA USHIRIKIANO KATIKA UJENZI WA WAHUSIKA

### 3.1 Utangulizi

Katika sura ya tatu kanuni za utaratibu wa ushirikiano zimechunguzwa ili kudhihirisha jinsi zinavyosaidia kujenga wahusika katika *mama ee*, kanuni hizi zimeweza kukiukwa kwa kiasi kikubwa ni kutokana na hayo utafiti huuhauna budi kutoa maelezo kuhusiana ukiushi huu,ukuushi wa kanuni hizi huwa na lengo moja kuu ambalo ni kuendeleza utaratibu wa ushirikiano wakati wa mazungumuzo, katika kufanya hivyomazungumuzo hayakatizwi na hivyo mawasiliano kufanikiwa.

### 3.1.1 Ukiushi wa Kanuni ya Idadi

Kanuni ya idadi ina sema kuwa msemaji anapaswa kusema yale ambayo yanatosheleza na yasizidi kiasi wala kupunguza taarifa ili kuweza kuwasiliana kwa njia mwafaka. Habari inayosemwa yafaa iwe kamilifu. Itafanyika hivyo ikiwa mzungumzaji amezingatia kanuni hiyo. Kwa upande mwingine msemaji atakuwa hana budi ila kuivunja au kukiuka kanuni hii. Huenda msemaji akatoa habari zaidi na yaliyotarajiwa au kidogo kulikoa kiasi cha kawaida. Katika kufanya hivyo huwa anafanikisha mawasiliano ili wawe na uelewano mzuri. Mifano kutoka *Mama ee.*

Mhusika mkuu Mwavita ameonekana kuwa wa kusema sana. Hali hii inamfanya tumuelewe kama mhusika ambaye ana msimamo dhabiti dhidi ya kauli yake. Ni kutokana na kusema kwake sana tunapata kutambua jinsi mwanamke amesawiriwa katika *Mama ee.* Mwavita anapoulizwa swali na mumewe, hamjibu moja kwa moja. Mwavita ana hakikisha kuwa ametoa maelezo zaidi ya yale yanayotarajiwa hivyo kumfanya Kinaya kupata kumwelewa zaidi. Kwa mfano:

Kinaya: Wanitukana siyo? Yaani mimi si mume?

Mwavita: Mume gani asiyejua kwalika nini nyumbani kwake au mkewe avaa nini, taa maji kila kitu nalipia mimi. Wewe zako ukinge na kwenda ulevini. Urudi usiku wa manane na matusi tele kinywani. Ati mwanaume-wanaume

walikuwa zamani za babu zetu- Ela nyinyi…..(uk 4)

Badala ya Mwavita kumjibu Kinaya kuwa wewe ni mume au wewe si mume, amedokezea mengi ambayo pale mwisho anaposema kuwa "*wanaume walikuwa zama za babu zetu"*. Hili ni jibu tosha kwa Kinaya kuwa yeye si mume. Hawajibiki kama wafanyavyo waume. Hapo basi tukapata kuelewa kuwa majukumu yote kawachiwa mwanamke. Mwavita akawa mwenyewe msimamo dhabiti. Mama pia ameweza kukiuka kanuni hii ya idadi. Katika kufanya hivyo anamtaka Tenge aweze kumwelewa kuwa katu hatamuacha. Kwa mfano.;

Tenge: Lakini mama umenisamehe?

Mama: (*Akimkumbatia*) Hata nikikasirika wewe bado ni mwanangu. Nilikubeba mwangu mwilini miezi tisa kutimia. Ulinyonya langu ziwa miaka miwili nilikubeba mgongoni, nilikuogesha, nilisikia kwa furaha tamshi lako la kwanza. Nilikuuguza kila aina ya magonjwa! Huo mwanangu ni mwungano usiowezekana kuvunjika. Mwanangu nikwambie nini, ngojea miezi michache utaelewa maneno yangu.(uk 18)

Ukweli ni kwamba kutokana na swali la Tenge "lakini mama uenisamhe?" jibu lake lingekuwa "ndiyo mwanangu nimekusamehe" au "la mwanangu sitakusamehe. Lakini kutokana na maelezo ya Mama kwake Tenge, anampa hakikisho tosha kuwa katu yeye na mtoto wake hawawezi wakatenganishwa na hivyo anamhakikishia msamaha wake. Hivyo basi mama akasawiriwa kuwa mwenye kusamehe na mwenye kupenda mtoto wake.

Katika mazungumzo yake, Mwavita na Tenge ni wazi kuwa Mwavita akiuka kanuni ya idadi, kwa sababu hamjibu Tenge moja kwa moja anavyomuuliza. Anatoa maelezo marefu ambayo mwishowe yanaashiria kuwa alikuwa anataka madafu. Katika kukiuka kanuni hii ya idadi, Mwavita anasawiriwa kama mpole. Kwa mfano;

Tenge: Ni mwenye madafu. Ninunue?

Mwavita: Nitakunywa kidogo. Kichwa changu kimetulia kidogo,nunua yaliyokomaa kidogo ndiyo matamu.

Kwa upande mwingine Mwavita anakiuka kanuni hii kwa kusema yaliyo machache mno. Hadi kumfanya mtu aweze kufanya utafiti wa ndani ili aweze kupata alilomaanisha. Kwa mfano;

Kinaya: Kwani una nini wewe?

Mwavita: *(aketi wima kitini kwa hasira)* Ulichonipa! (uk 64)

Jibu lake Mwavita lina utata. Huenda Kinaya amempa vitu vingi vikiwemo pesa, nguo na vinginevyo. Alimaanisha nini haswa aliposema *"ulichonipa".* Hapa ninapata maana kuwa ni ujauzito. Hivyo alikuwa na hasira sana na kumfanya kuwa mwanamke mwenye hasira nyingi.

Kuvunjwa kwingine kwa kanuni ya idadi ni pale Tenge anapomuonyesha Padre kuwa hamna lolote wanaweza kusema na Kinaya kwa sababu wote hushiriki mvinyo. Badala ya Padre kujitetea kuwa huwa hawanywi na Kinaya, jibu lake ni la maelezo marefu ambapo hata anamkumbusha Tenge kuwa mtoto wake ni haramu, hivyo hastahili kubatizwa. Padre kama mhusika amesimama kwa niaba ya dini ya kikristo ambapo watu humuona kuwa mtakatifu na nayekaribia Mungu. Padre kama mhusika, kutokana na jibu lake tunapata kuwa amesimamia wale mapadre ambao huvalia tu majoho yao ilhali hawana chochote kuhusu Mungu. Ni wa kujificha katika dini tu ni padre laghai. Kwa mfano:

Tenge: (*Kwe bezo*) Twambie jingine, Padre wa Mungu! Alikununulia chupa ngapi? Na Mwavita akirudi, atakunulia ngapi zaidi?(uk 83)

Padre: *(Kwa hasira)* Unatukana kazi ya Mungu. We! nyamaza. Huyo mwanao hajabatizwa na hatabatizwa kwa ajili ya kosa lako wewe. Usitie mkosi hapa. Usifukuru ukajipalia makaa ya moto.

Kutokana na jibu la Padre, ni wazi kuwa amekasirika kwa sababu kumbe matendo yake yanajulikana. Hivyo ni ukweli yeye hushiriki mvinyo. Ikawa ni vigumu kwake kukubali moja kwa moja. Kutokana na jibu lake ni ukweli kuwa yeye ni Padre laghai.

### 3.1.3 Ukiushi wa Kanuni ya Uhusiano

Kanuni ya uhusiano inaweza kuvunjwa pale ambapo msemaji ameonelea kuwa yatakayosemwa yatawaathiri wasikilizaji na yatakuwa kinyume na matarajio. Mara nyingi ukiushi huu hutokea pale ambapo jibu la swali huwa haliambatani na swali liliolizwa. Kwa mfano Kinaya na Mwavita wakiwa wahusika wakuu, wameweza kukiuka kanuni ya uhusiano pale ambapo wanaonekana kukizana katika majibu yao. Ukiushi huu umemjemga Mwavita kama mhusika mkuu anayepitia mateso katika *Mama ee.* Ni kutokana na ukiushi huu wa uhusiano tunapata kuelewa yale yote ambayo Mwavita anapitia. Pia inatusaidia kumsawiri Kinaya kama mume ambaye anamtesa mkewe. Kwa mfano;

| | |
|---|---|
| Kinaya: | Ulikuwa na nani hapa ndani nilipoanza kubisha? Ee sasa umemkasirikia nani? Ee? Ni nani sasa? Una nini? |
| Mwavita: | Sina lolote nakuona wewe unayenishukia kwa vishindo saa tisa za usiku au asubuhi bila kuniuliza hali! Mmh! Kinaya we! Kumbe ile *I love you*-nakupenda Mwavita ndipo ilipoishia kabla ya miaka mitatu kuisha lo!(uk 3) |

Jibu la Mwavita “kumbe ile I love you –nakupenda...” lina maana kuwa wakati mwanamume anapomuona mwanamke, huwa kuna mapenzi ya mwanzoni ambayo huwa tu ni ya muda. Wakati mume anapotambua kuwa sasa ameoa anabadilika na kuwa si wa kumpenda tena mkewe. Hapo ndipo huanza kumdhulumu mkewe. Hivyo basi Mwavita hakutaka kmwelezea wazi wazi kulingana na maswali yake.

Matamshi ya Kinaya pia yameweza kukiuka kanuni ya uhusiano kwa kumuita Mwavita hawara. Mwavita haamini mambo haya yana ufafanuzi zaidi. Maneno hayo yanamkera ikichukuliwa kuwa aliolewa kwa Kianya akiwa bado bikira. Alipotaka Kinaya aelezee vizuri, Kinaya aliweza sasa kugeuza na kumzungumzia Tenge. Hii ni kwa sababu huenda mambo yangekuwa mabaya sana na pengine kukatiza usemi ambapo sasa angekuwa amevuruga utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo. Kutokana na kauli hii, tunapata kumsawiri Kinaya kama mume aliye na

madharau na ambaye hampendi kamwe mkewe. Ni mume ambaye humdharau mke baada ya kumuoa. Kwa mfano:

Mwavita: *(Amesonga mbali)* Wewe ulinioa nilipokuwa mwanamwali sasa ushanifanya mama waniita hawara! Aah! Kinaya ndugu yangu! walidharau hivyo?

Kinaya: Tenge dadako si hawara? Siku zote George ananipeleka sinema-twende ngomani. Ngoma hiyo tutaiona mwisho wake.”Matamshi yake Tenge yanazingatia kanuni ya uhusiano. Alipoulizwa na mama yake aseme alichotaka msichana hakusita. Alimwelezea ukweli bayana. Tenge alifanya hivi aweze kuendeleza mazungumzo na mama yake. Katika kufanya hivi amesawiriwa kama mwanamke ambaye ni jasiri na mbaye yu tayari kusema ukweli hata kama ukweli huo utaumiza. Tenge hapo akasema ukweli.

Mama pia amekiuka kanuni ya uhusiano. Alivyomjibu Tenge “ mwanangu kua ujionee mwenyewe” alimaanisha kuwa waume ni watu wabaya ila hakutaka kusema hivyo moja kwa moja akaonyesha kuwa mumewe ni mbaya.

Pia mama hakutaka kumwonyesha Tenge kuwa baba yake ni mbaya, kwa sababu angekuwa anavunja uhusiano wao. Kutokana na jibu lake mama “mwanangu kuja ujionee mwenyewe” tunaweza kumsawiri kama wale wanawake ambao ni wanyonge wamenyanyaswa na waume zao wakawa hawana wa kuwatetea na kubaki kudhulumiwa tu. Kwa mfano

Tenge: Na baba je?

Mama: Mwanagu kua ujionee mwenyewe.(uk 18)

Kinaya pia amekiuka kanuni ya uhusiano. Alipoenda kwa kina Mwavita, hakufanya kulingana na utamaduni na mila za kule. Ilikuwa ni jukumu lake kwenda huku awe amemnunulia nyanya yake Mwavita zawadi. Jambo hilo hakulitekeleza. Wakati nyanya yake Mwavita alimuuliza ni lini alitoka mjini, hakutarajia jibu lile. Alitarajia Kinaya amkabidhi zawadi aliyomnunulia. Kinaya kupeana jibu lile, anasawiriwa kama mume ambaye amepotelea katika elimu ya sasa ambayo

imemnyima nafasi ya kushughulikia na kuzitambua mila na desturi zao. Kwa hivyo Kinaya ni mwacha mila. Kwa mfano:

Nyanya: (*Akisema na Kinaya*) Umekuja lini bwanangu kutoka mjini?

Kinaya: (*Anaonekana mwenye haya*) Nimekuja leo asubuhi ya saa tano.

Nyanya: *(Akiwageukia wote walioko)* Mnawaona mabwana wa leo. Hata hakumbuki bibi yake wa kwanza.(uk 22)

Mwavita ameweza kuzingatia kanuni ya uhusiano. Kwa mfano katika kikao chao cha kuwakosoa na kuwaleta pamoja, Mwavita anaonekana kusema ukweli wa mambo yalivyo. Katika kufanya hivyo anasawirika kama mwanamke msema ukweli na ambaye ameyapitia mengi huku akionyesha uvumilivu. Aliliuzwa anajibu kwa njia bora ili aseme yote anayopitia, hasiti kamwe. Anataja makosa yale yote Kinaya humfanyia hivyo kuwawezesha wazee wa wazazi wa pande zote mbili kuweza kutambua ubaya unatokea wapi.

Kinaya anaendelea kukiuka kanuni ya uhusiano. Kipengee hiki “wazee wamenieleza makosa” kinatusaidia kumsawiri kama mwanamume aliyejaa madharau hata kwa wazee wake kwa sababu ya elimu na cheo chake kazini. Kwa mfano;

Ba mkubwa Kinaya: Kinaya jibu swali hilo mwenyewe, sisi hatuwezi kuisoma akili yako tukajua fikira zako juu ya yote yalisemwa.

Kinaya: Wazee wamenieleza makosa.

Kutokana na jibu la Kinaya kuwa “wazee wamenielza makosa” anaonyesha kuwa hana kosa lolote ila ni wazee wamesema kuwa ndiye mkosaji. Ndipo tunamuona kuwa mwenye madharau na wa kutoheshimu wakubwa wake.

Padre ni mhusika mwingine ambaye pia amekiuka kanuni ya uhusiano. Kwa kuwa yeye ni wa dini, hataki kuonekana kama kwamba anaiasi dini kwa kusema ukweli wa mambo au kwa kukubaliana na kauli fulani. Mwavita na Kinaya pia wamekiuka kanuni ya uhusiano. Wakati

Kinaya anawatembelea Mwavita na Tenge baada ya kutalikiana, tunawaona katika mazungumzo yao hawelengi kabisa kinachoendelea. Kwa mfano Kinaya anapojulia Mwavita hali, Mwavita kwa upande mwingine hamjibu kuligana na lile swali. Katika kufanya hivyo tunamsawiri Mwavita kama mwanamke aliyejaa hasira na hamaki kwa jinsi vile korti iliamua kunyume na matarajio yake kwa kumpa Kinaya mtoto. Haonekani kushawishika hata anapoambiwa kuwa kila mara mtoto anamuulizia. Mwavita angekuwa kama wanawake wengine, angeshikwa na huruma na kuamua kumrudia mumewe ili aweze kuwa karibu na mtoto wake wa pekee. Ni mwanamke ambaye katu habadilishi msimamo wake. Kwa upande mwingine, Kinaya anonekana kama mwenye madharu, na ambaye anaonekana kuwa ana ushawishi mkubwa kwa korti na polisi. Licha ya yeye kuambiwa na mahakama kwamba asimtembelee Mwavita auasipatikane karibu na makazi yake, yeye anavunja sheria hiyo na kushika njia hadi kwa Mwavita. Ni kutokana na haya tunamsawiri kama mwanamume aliyejaa madharau na kiburi kutokana na pesa na cheo alichonacho kazini. Kwa mfano;

Kinaya: Habari za jioni mpenzi? Mbona husemi waziba masikio? Mpaka sasa hujanisamehe?

Mwavita: Kwanza kimekuleta nini hapa? Ulivyoambiwa na hakimu huyajui tena? Ushahonga polisi wote wasikuzuie kwenda kokote hata kama kinyume cha sheria? Kwenda huko.

Kinaya: Polisi gani? Watanishikaje? Kwani hujui cheo changu cha sasa? Polisi hawawezi kucheza na mimi?

Mwavita: Sasa wataka nini hapa? Kimekuleta nini hapa?

Kinaya: Mwavita ndugu yangu, naona umestarehe sana! Lool! Gari, nyumba nzuri,imepambwa ikapambika.

Kutokana na “ushahonga polisi wote wasikuzuie kwenda kokote hata kama kinyume cha sheria. Kwenda huko” Mwavita ni mwanamke ambaye kwa kupitia mateso mengi huku akivumilia, hataki kamwe kurudia hali ile. Mwavita amekata kauli na hivyo hataweza kuenda kinyume na kauli yao. Kinaya naye ni mwenye kiburi na madharau. Hivyo anaona kuwa akija huku akijidai kuwa ana cheo kikubwa ataweza kumshawishi Mwavita arudiane naye.

### 3.1.3 Ukiushi wa Kanuni ya Ukweli

Kanuni ua ukweli inamtaka msemaji aseme kile kilicho cha ukweli. Habari zitakazotolewa na msemaji ziwe za ukweli na hivyo basi msemaji asiseme habari ambazo anaamini ni za uongo au habari ambazo hana uhakika nazo. Ikiwa msemaji atasema, basi ahakikishe anasema kile ambacho anaweza kudhibitisha. Awe katika nafasi bora ya kutolea ushahidi yale ambayo amesema. Katika kufanya hivyo msemaji atakuwa anazingatia kanuni ya ukweli. Kwa upande mwingine kanuni hii huenda ikakiukwa. Sababu za kufanya kanuni hii kukiukwa ni kama vile heshima, kutovuruga matarajio ya wanajamii, kuzingatia upole na vilevile kuweza kufanya mawasiliano yaendelee bila kukatizwa. Katika *Mama ee,* wahusika wameweza kwa kiwango kikubwa kukiuka kanuni ya ukweli. Hivyo basi ninataka kuchunguza ni kwa kiasi kipi kanuni ya ukweli imevunjwa na kutoa sababu ambazo ndizo umaanisho na kuweza kuchambua tabia za mhusika baada ya kuvunja kanuni ya ukweli. Kwa mfano;

> Kinaya: Ondoka hapa. Wafikiri wewe ndiye mwenye uchungu wa mtoto peke yako? Juma ni mwanangu hilo nina hakika nalo. Huyo atakayemfuata ndiye sina hakika naye maana siku hizi umekuwa kigunjia.(7)

Katika mazungumzo haya Kinaya anataka tutambue kuwa hata kina baba waujua uchungu wa mwana. Jambo hili hana uhakika nalo kwa sababu haelewi kamwe wakati mzazi hutumia methali hiyo huwa anamaanisha nini. Yeye ni kati ya wale waume ambao hujigamba kuwa wana watoto ilhali hawatambuia jinsi ya kugaramia mahitaji yao. Pili ni kwa jinsi gani atasema kuwa ana uhakika kuwa Juma ni mwanawe halali? Hata kama alimpata Mwavita akiwa angali bikira. Kutokana na usemi wa Kinaya, yeye ni mwanamume wa kujigambia watoto ambao hata hajui hatambui wala nini na wavaa nini. Ni mwanamume kwa jina tu.

Mwavita ameweza kukiuka kanuni ya ukweli. Pale ambapo anajibizana na Kinaya, hamwambii ukweli wa mambo ulivyo. Anaposema kuwa Kinaya ametelekeza mwanawe,hasemi kwa uwazi kuwa majukumu ya mtoto amewachiwa na Kinaya. Ana uhakika kwa sababu ametwikwa jukumu la kumlea pekee yake kana kwamba hana mume. Anampa mumewe uwazi kuwa mtoto bila kushughulikiwa hamna vile mtu atasema ni wake kwa vile ndiye anaaminika kuwa baba ya mtoto yule. Katika kufanya hivyo tunampata Mwavita kuwa mwanamke mvumilivu na mwenye

bidii. Ameweza kuvumilia mateso ya Kinaya na huku akatia bidii kuhakikisha kuwa mtoto wake anapata lishe na mavazi hadi elimu na makazi pasopo kusaidiwa na mumewe. Kwa mfano;

> Mwavita: Wacha utoto hapa. Mtoto wako jina tu. <u>Kwa kuwa siku koja ulijifurahisha kwangu. Hilo ndilo tu linalomfanya kuwa wako</u>. Wajua raha yake tu taabu zote juu yangu mimi. Mimi ndiye mwenye uchungu wa mwanangu.(uk 8)

Ni mhusika ambaye ameweza kukiuka kanuni ya ukweli. Wakati anaelezea wazee alichowaitia, haneni maneno ya ukweli. Kwa mfano anaposema kuwa bado mtoto wao alikuwa anapenda mkewe, je hilo ana uhakika nalo? Hili ni jambo hawezi kudhibitisha mbele ya wazee. Kwa sababu haishi katika nyumba ya Mwavita na Kinaya akapata kujua kile kilikuwa kikiendelea. Katika kufanya hivyo, anatambulika kuwa mzazi ambaye humficha mtoto wake hata baada ya kutenda maovu ambayo yameshuhudiwa na wengi. Hataki watu waone kuwa mtoto wake Kinaya ni mbaya. Ba mkubwa Kinaya ni miongoni mwa wahusika ambao ni wa kufunika uozo wa wana wao ili wasidhalilishwe. Kwa mfano;

> Ba mkubwa Kinaya: Sisi mjomba tumewaita maana mtoto wetu amesema bado anampenda mkewe na amtaka warudiane, tunajua kuwa.(uk27)
>
> Ba mkubwa Kinaya: Juzi mambo yaliharibiwa na kutoelewa mila zetu. Huyu mwanangu amekulia shuleni na baada ya hapo akasomea ng'ambo na kurudi hapa aliandikwa kazi mjini.(uk 28)

Kinaya pia ameweza kukiuka kanuni ya ukweli anapoulizwa aseme alichomfanyia Mwavita hadi akaamua kumtoroka, basi hapo tunamuona akisema uongo kwa vile hataki wazee wamuone alivyo mnyama. Hataki wamtambue kama mume ambaye ni wa kumtesa kwa kumpiga mkewe kila wakati. Kinaya ni mwanaume katili.

Huyu ni miongoni mwa wanaume ambao ukiwaona kwa nje ni wazuri ilhali wameficha tabia zao mbaya za ukatili kwa kusema uongo.Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| Kinaya: | Kulitokea ubishi kati yetu Juma alipokuwa mgonjwa. Mwavita alikasirika kwa kuwa hakunipata ofisini na ikamlazimu yeye kumpeleka mtoto kwa daktari. Niliporudi nyumbani jioni alianza kunitukana na kusema kuwa simjali yeye wala Juma. Mwisho nilikasirishwa na matusi yake kwangu na kumpiga kofi. Tulisukumana naye mwisho alianguka na kung'oka meno mawili.(uk 36) |

Maneno haya ya Kinaya si kweli. Kwa sababu ikiwa Kinaya hakuwa ofisini wakati wa kazi, alikuwa ameenda wapi? Na je hili ndilo jambo la kusababisha kupigana kwao? Hataki kusema ukweli kuwa alimpiga Mwavita konde ambalo lilingo'a meno yake mawili. Hataki kuingiliwa zaidi hivyo kuficha ukweli wa mambo. Kinaya pia kwa kukiuka kanuni ya ukweli, anasawiriwa kama mwanamume mjeuri sana. Hii ni kwa sababu anaonekana kukerwa na yale mke wake anayasema ambao ni ukweli bayana. Kwa mfano;

| | |
|---|---|
| Kinaya: | Sina mke niliyemweka na jambo hilo tushalizungumzia tukalimaliza mimi na........ |
| Mwavita: | Sijui kwa nini amelitea hapa! |
| Mzee wa kijiji: | Ni kwa kuwa leo ni siku ya kutua moyo nimemwomba aseme yote asifiche ndiyo maana amesema. Ni kweli aliyosema? |
| Kinaya: | Kwa sasa si kweli. |

Nyanya pia amekiuka kanuni ya ukweli. Hataki kuwaambia wazazi wa upande wa Mwavita na Kinaya hawajawajibika kuwaelimisha watoto wao. Hana uhakika ikiwa kuna upande umeelimisha mtoto wao. Anapofanya hivyo tunamuona kama mhusika ambaye anapenda amani. Huenda katika mazungumzo hayo anatambua upande ule ambao una makosa. Kwa vile hataki kuonekana kama wa kuchochea upande mmoja, basi anawajumlisha wote. Pia anatambulika kuwa mwenye busara, kwa vile katika kupatanisha watu huwa si vizuri walio wakongwe kuegemea upande mmoja. Hataki kuvunja umoja na upendo ulioko kati ya familia hizi mbili. Kwa mfano;

> Nyanya: wasichana wamekuwa kama wanyama wanatupa watoto mapipani, wavulana waua, wapiga wake. Msimlaumu Kinaya pekee katika kisa hiki. Nyinyi wazazi hamkutimiza jukumu lenu kikamilifu kwa watoto wenu. (uk 48)

### 3.1.4 Ukiushi wa Kanuni ya Namna/Jinsi

Katika kanuni hii msemaji anapaswa kusema mambo yaliyo bayana, wazi na yaliyo dhahiri bila kuficha chochote. Ujumbe usio na utata, uwe na mpangilio na utaratibu mzuri aidha uwe mfupi, lugha inayotumika pia lazima ieleweke na msikilizaji wake bila tatizo lolote. Mara nyingi kanuni hii hukiukwa na wazungumzaji wengi. Sababu kuu ya kukiukwa kwa kanuni hii ni kuwa kusiwe na kuvunjwa kwa utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo. Hivyo basi kufanya mazungumzo yaendelee. Kwa kuzingatia mifano katika *Mama ee,* tunachunguza kwa kiwango kipi wahusika wamekiuka kanuni hii na ni kwa jinsi gani ukiushi huu umesaidia kujenga uhusika wao.

Mwavita amekiuka kanuni ya namna kutokana na vile anavyozungumza, inaonyesha kuwa anayashughulikia makjukumu hayo peke kaye. Katika kufanya hivyo tunamuona kuwa ni mwanamke ambaye ameolewa ndio lakini hafurahii ndoa yake. Anatuacha na maswali mengi kuwa anaamanisha nini anaposema *“kweli wengine tumeolewa!”* ilhali tunamuona akiwa katika ndoa yake. Mwavita anajitokeza kuwa mwanamke ambaye anajutia ndoa yake kinyume ilivyo na matarajio ya wengi wanapoolewa. Kwa mfano;

> Mwavita: (*Akinung’unika kuangalia saa yake mkononi*) Lahaula! Saa tisa za usiku. Saa hizi ndipo laja! Aha, <u>kweli wengine tumeolewa!</u> Mchana kutwa nimezurura kutafuta waganga na waganuzi sina wa kunisaidia ni kama niliyefiliwa na mume au niliyezaa nje ya ndoa- ilhali jiume lenyewe levi lazurura na mgongo wa gari likibadilisha wasichana kama mashati.(uk 1)

Mwavita pia kutokana na malamishi yake, tunamsawiri kama mwanamke aliyejaa upweke. Hii ni kwa sababu Kinaya ambaye ni mume wake, haonekani kuwa karibu naye hivyo kumtwika majukumu yote ya kinyumbani.

Kinaya pia amekiuka kanuni ya namna. Kutokana na vile anavyomwashiria Mwavita ni wazi kuwa ni mwanamume mwenye madharau kwa mke wake. Anaonekana kuwa hathamini mke wake, hivyo basi anatumia hali ya ukubwa katika sentensi kuthibitisha hayo. Kwa mfano;

> Kinaya: Jike gani hili nililoowa! Kunifungulia mlango taabu na hata niingiapo ananitazama kama niliyetapakaa mavi! Nilichobeba hatizami.(uk 3)

Kutokana na malalamishi yake Kinaya, tunamuona kuwa mwanamume ambaye amejaa ubabe dume. Yeye ni kuamrisha na kutaka kushughulikiwa bila kujali wale wanaomshughulikia hali zao ziko vipi?

Baba pia amekiuka kanuni ya namna. Ni kutokana na kusema kwake, tunapata kutambua kuwa ni mzee ambaye hawezi kurudi nyuma akiwa amekwisha kata kauli. Hataki kabisa kusikiza Tenge akimuomba kuwa amsamehe kwa sababu lilikuwa kosa la siku moja. Ni wale wazee ambao ni wakali mno hadi hawawezi kuchukua fursa ya kumsikiza mtu na kuweza kusamehe. Amejaa ubabe dume. Ndipo hata anaashiria kuwa Tenge kupata ujauzito ni kwa sababu ya mama yake kukosa kumpa mafunzo. Baba hapa ni mwanaume ambaye pia ametwika mama mzigo wa kulea, kushauri na kutunza watoto wake. Kwa mfano;

> Baba: (kwa mabezo na kuiga) Kosa la mara moja Nisikuone nyumbani kwangu tena (Tenge alia zaidi). Toweka kabisa mbele ya macho yangu na usiniite tena baba. Kosa la mara moja! kwani hukujua mwisho wake? Huyo mamako hakuwaambia? (uk 15)

Nyanya pia ni mhusika ambaye amekiuka kanuni ya namna. Anapofanya hivyo hataki kabisa kuonekana anawakosea heshima watu wa kutoka kwa kina Kinaya. Lakini hata baada ya kusema hayo ni wazi kuwa alikuwa anampa Kinaya mafunzo na kumuonyesha kuwa alikosa kuja kwa kina mkewe akiwa mlevi. Nyanya hapa anasawiriwa kuwa mwenye busara na mpenda amani na utangamano mwema. Kwa mfano;

> Nyanya: Zamani zetu sisi sheria zilikuwa zikifuatwa sana. Kamwe haikuwezekana mtu kuwa mlevi na kuenda kwa mkwewe. Pili mametu huheshimiwa

> lakini mama huyu aliyemzaa mke aliyemwoa huyo ndiye anayepewa sana sana heshima, ndiyo maana huwezi hata kula mbele yake ya kupita karibu naye au kumgusa kwa hivyo yaliyofanyika mbele yake ni makubwa sana. Kama nimekosea wanangu watasema na huyu babangu atasema.(uk 30)

Mjombake Mwavita pia amekiuka kanuni ya namna. Anaonekana kukasirishwa na matendo ambayo Mwavita amekuwa akipitia katika ndoa yake. Hivyo basi anapozungumzia suala la kutoza Kinaya faini, hataki kutumia maneno yenye ukali. Anapunguza ukali huo kwa kutumia jazanda. Ni kutokana na haya tunamuona ni mtu ambaye pia ana heshima na ni mpenda amani. Hataki kuonyesha waziwazi kuwa amekasirika, pia hataki kutumia maneno yenye ukali licha ya yeye kuudhika na yale ambayo anapitia Mwavita. Hivyo basi tunamuona akiwa mpole. Kwa mfano;

> Mjombake Mwavita: Hiyo ndiyo mila hasa. Kila kosa lina fimbo yake. Fimbo isipokuwa kali ya kutosha, mtoto atarudia tena kosa hilohilo au atende baya zaidi.(uk 33)

Kwa ufupi mjombake Mwavita alikuwa anamaanisha kuwa adhabu au faini atakayopewa Kinaya, iwe kubwa kulingana na makosa aliyotenda hivyo asiweze kuridua makosa hayo. Ba mkubwa Mwavita kwa kuvunja kanuni ya namna, tunamsawiri kama mhusika aliye na hasira hasa pale ambapo haambiwi ukweli wa mambo. Ni mhusika ambaye atapinga uwongo wowote ule ambao utajotokeza wakati msemaji anapoongea. Yeye hana subira. Papo hapo atakabiliana na mtu kwa maneno wakati ambapo hajaridhika. Kwa mfano;

> Ba mkubwa Mwavita: Wacha! Wewe na Mwavita mwaweza kusukumana na kupigana? Mwavita huyu awezaje kusukumana na jitu kama wewe muo..(uk 36)

Ba mkubwa Mwavita alimaanisha kuwa hakuna vile mwanamke mjamzito anaweza kusukumana na jitu kama vile Kinaya hadi wakaangushana chini na kumfanya kupoteza meno yake. Ba mkubwa Mwavita anataka Kinaya azungumze ukweli wa mambo.

Mzee wa kijiji ni mwenye busara, hapendi ugomvi wowote ule. Mzee wa kijiji anaelewa wazi yale Mwavita anapitia katika ndoa yake. Anamshawishi kuyasema yote. Katika kufanya hivyo anatumia lugha ya kubembeleza ya kufanya Mwavita ambaye amejaa hasira na huzuni kuweza kusema yote. Kwa mfano;

> Mzee wa kijiji: Eleza yote mke wangu. Usibakishe kitu kikakukera moyoni. Leo ni siku ya kufua moyo usibaki na undani wowote na mtu yeyote.Usiogope maana walio hapa wote ni jamaa zako, baba, mama, nyanyako. Hakuna mtu wa mbali. Sema yote.(uk 38)

Mzee wakijiji pia ni wa kubembeleza na kuhakikishia watu kuwa yote yako sawa. Anamuonyesha Mwavita kuwa asiwe na wasiwasi kwa sababu walioko pale ni watu wa jamaa na wako tayari kumsaidia. Mwavita kwa kiasi kikubwa ameweza kuzingatia kanuni ya namna.katika kufanya hivyo, anataka walio katika kikao cha kuwasikiza waweze kumwelewa vizuri ili wasiwe na shaka na yale ambayo anapitia katika ndoa. Hamna yeyote ambaye ametatizika kupata kuelewa alichokuwa akisema Mwavita. Mwavita hivyo basi ni mwanamke mwenye kuteswa katika ndoa katika hali zote, za kisaikolojia, kupigwa na kata kufanywa kukosa kufikiri vizuri. Mwavita pia ni mwanamke mwenye msimamo dhabiti. Kwa mfano anapoulizwa na mzee wa kijiji ikiwa atamrudia Kinaya anajibu hivi.

> Mzee wa kijiji: Mwanangu, mke wangu tumesikia taabu uliyopata na kuwa wewe mjeuri. Kabla ya kuendelea zaidi nitakuuliza swali moja. Utamrudia bwanako au ndiyo humtaki kabisa?
>
> Mwavita: Babu, mtu hamwoni nyoka mwenye sumu, aliyemuuma siku moja, akarudi tena kumkanyaga!(uk 49)

Mwavita anaonyeshwa hapa kuwa ni mwanamke mwenye heshima na mwenye msimamo dhabiti. Kutokana na usemi wake alimaanisha kuwa kamwe harudi. Njia aliyotumia kutolea jibu hilo ni ya kutatanisha ambayo inamtaka mtu kufanya uchambuzi wa ndani. Ikiwa angeweka jibu lake waziwazi basi, hapo angekosea heshima wale wazee. Ndipo akamua akakataa kwa kutumia njia ile katika kutoa kauli yake.

### 3.1.5 Hitimisho

Sura hii imedhihirisha kuwa umaanisho umesaidia kuwasawiri wahusika. Hii ni kutokana na kuchunguzwa kwa mazungumzo ya mhusika na kubaini ni kipengee kipi katika mazungumzo yake ambacho kimeibua umaanisho kwa kukiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano. Matokeo yake ni kuwa, kwa vile utafiti ulijikita katika kuchunguza lugha kwa ujumla inavyotumiwa na wahusika, hivyo basi kubaini ni sehemu ipi inayozua umaanisho na hivyo kumpa mhusika sifa zake.

## SURA YA NNE

## UMAANISHO KATIKA UKUZAJI WA MAUDHUI

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inachunguza mchango wa umaanisho katika ukuzaji wa maudhui ya ndoa,utamaduni, ubaguzi wa jinsia ya kike,dini na umoja wa akina mama katika kufanya hivyo, utafiti huu utajikita katika mazungumzo ya wahusika ambayo yanazua umaanisho na hivyo kubaini ni maudhui yapi yanayojitokeza.

### 4.1 Umaanisho na Ndoa.

Muungano wa maisha kati ya watu wawili, mume na mke ni ndoa ambao unakubaliwa na kuheshimiwa na jamii. Kando na kuwa muungano wa watu wawili unaweza kuwa kati ya mtu mmoja ambaye ni mume na wengine zaidi wakiwa ndio wake zake. Katika *Mama ee* kuna ndoa kati ya mama na baba yake Mwavita ambayo tutaishughulikia kwa kuangazia ni kwa jinsi gani umaanisho unavyojitokeza. Pia kuna ndoa kati ya mama na baba yake Kinaya ambayo haitashughulikiwa. Ndoa kati ya Mwavita na Kinaya ndiyo imetuwezesha kuangazia jinsi umaanisho unavyojitokeza na kusaidia kujenga maudhui haya.

Ndoa kati ya Mwavita na Kinaya imejaa misukosuko mingi, hakuna kuelewana na hamna anayemthamini mwenzake. Ndoa hii ni ile iliyofungiwa kanisani kwa misingi ya kanisa la Kikristo ambayo inamhitaji mume kuwa na mke mmoja na waishi katika upendo na kusaidiana katika hali zote. Haya tunayaona yakipuuzwa katika ndoa hii. Kutokana na kulalamika kwake Mwavita katika ukurasa wa kwanza kuhusu jinsi alivyomushughulikia mtoto wake pekee yake ni wazi kuwa ndoa yao haiendi vizuri .Kwa mfano;

> Mwavita: ..........mchana kutwa nimezurura kutafuta waganga na wanganguzi sina wa kunisaidia-ni kama niliyefiliwa na mume au niliyezaa nje ya ndoa –ilhali jiume lenyewe levvi lazurura na mgongo wa gari ukibadilisha wasichana kama mahati (uk 1)

Umaanisho unaojitokeza kutokana na mazungumzo ya mwavita “--------ni kama niliyefiwa na mume au niliyezaa nje ya ndoa,’’ni kwamba wanaume hawajali kabisa wake na watoto wao. Hivyo basi Mwavita ndiye wa kushughulikia mtoto bila usaidizi kutoka kwa mumewe.

> Kinaya: “(*akilalamika*) Jike gani hili nililoowa!kunifungulia mlango taabu na hata niingiapo----(uk3)

Fungu hili la maneno “jike gani hili nililioowa!” linatupa umaanisho kuwa heshima haimo tena katika ndoa ya Kinaya na Mwavita. Hii ni kwa sababu maneno hayo yametumika katika hali ya ukubwa ambayo ni ishara kuwa kuna kudharauliwa na kukosa heshima katika ndoa yao.

Heshima haimo tena katika ndoa hii Kinaya anamdharau sana Mwavita na kumtesa hivyo basi hata anamtaka ampikie chakula hata kama ni usiku wa manane na hata mapambazuko anapoingia. Hajali habali saa na wakati ila ni kutoa amri zake. Wakati watu huoana huwa mume anatozwa mahari ya kuleta muamala mwema katika ya familia hizi mbili. Lakini tunamuona Kinaya akiwa na maoni tofauti. Kwa mfano,

> Kinaya: Wao hawakulazimika kulipa pesa zaidi atii kwa kuwa mke ana shahada! Baba zenu, siku hizi wanawauza. Mimi nililipa shilingi elfu mbili zaidi kwa kuwa ulifika kidato cha sita. Wengine hulipa zaidi – si kununua nini?

Maneno haya “mimi nililipa shilingi elfu mbili zaidi kwa kuwa ulifika kidato cha sita,” yanazua umaanisho kuwa kuna kudharauliwa kwa Mwavita katika ndoa yao. Hivyo kuzua mgogoro kwa kuwa Mwavita anaona kudharauliwa kule, kumbe ni kwa sababu Kinaya anaona kuwa amemnunua kwa pesa. Maoni yake Kinaya ni kuwa mume anapolipia mke wake mahari huwa amemnunua. Wakati mtu hununua kitu huwa anakimiliki. Hivyo basi Kinaya anamuona Mwavita kuwa mali yake wala si mke wake. Hiyo ndiyo maana anamfanyia madharau yote hayo akijua kuwa hana pa kuenda. Hii inamaanisha kuwa ndoa za siku hizi zimekosa maana. Wakati watu wako mbele ya kanisa na kusomewa maandiko katika Biblia huwa ni kwa kufuata tu taratibu na hamna cha kutilia maanani. Pia mahari hayana maana katika ndoa za kisasa. Yamechukuliwa kama bei ya kumnunua mke hivyo basi huwa mke hana lake kwa kukumbushwa kuwa amelipiwa

mahari. Kwa hivyo kumfungia mwanamke katika ndoa na kumfanya kuwa mtumwa asiyekuwa na lake. Kwa mfano:

Mwavita: *(kwa dharau)* sahau sana enzi za mababu zako. Hii ni karne nyingine kabisa au wataka turudie enzi za mababu nawe uwe tayari kuishi kama mababu walivyoishi.

Kinaya: Una maana gani? Sikuambia urudie kuvaa ngozi au hando kama mabibi wa zamani. Nilichoomba kwako ni heshima na utii kwangu nikiwa mumeo wa ndoa.

Mwavita: Wala sikumwambia usivae suti yako. Vaa hata jua liwe kali namna gani mradi uujue na kuutimiza wajibu wako hapa nyumbani kama wewe mume kweli walivyokuwa mababu zetu.

Kinaya: Wanitukana sivyo? Yaani mimi si mume?(uk 6)

Katika mfano wanne, maneno yake Mwavita "......nawe uwe tayari kuishi kama mababu walivyoishi" "..... mradi ujue na kuutimiza wajibu wako hapa nyumbani kama wewe mume kweli walivyokuwa mababu zetu." Yanatupa umaanisho kuwa Mwavita ni wa kusema sana na hivyo anamkasirisha mumewe ambaye anaonelea kuwa kweli amedharauliwa. Mgogoro unapozuka una maan kuwa wanaume hapaendi sana kuzungumziwa kwa ukali na kwa mafumbo. Wakati hayo yanatokea basi huwa kunazuka mgogoro katika ndoa.

Kinaya: Sasa ulitaka nibebe mimba miezi mine unusu na wewe miezi mine unusu ndipo ukubali kuwa najua uchungu wake?

Mwavita: Wacha hoja za kipumbavu. Wajua waziwazi kuwa mimba hiyo ingeharibika kama si dawa. Hukumbuki ulivyonipiga teke? Kesho yake nilipolazwa hospitali nikiumwa ukasingizia ulevi! (uk 8)

Katika mfano wa tano, Kinaya anaposema kuwa "sasa ulitaka nibebe mimba miezi minne unusu na wewe mine unusu ndipo ukubali kuwa najua uchungu wake?" Haya yanatupa umaanisho kuwa wanauma wanaume wanapokiuka majukumu yao huku wakisingizia kuwa pia wao

wanaelewa uchungu wa mwana basi kuzusha migogoro katika ndoa zao. Umaanisho mwingine unao jitokeza kutokana na maneno yake Mwavita "hukumbuki ulivyonipiga teke?" ni kuwa wanaume wamejaa ubabe dume na hivyo kuwadharau na kuwatesa wake zao bila kujali hali za wake zao.

Ndoa ni ya watu wawili kuja pamoja, kusaidiana, kuelewana, kujadiliana ili kuendeleza ndoa yao. Lakini kutokana na lalama za Mwavita tunapata kuelewa kuwa haya yote yamekuwa ni kinyume cha matarajio. Mwavita ndiye amejitwika majukumu yote katika ndoa yao. Mumewe hajali jinsi ya kushughilikia mahitaji ya familia yake kwa kusingizia kuwa amemlipia mahari na tena hamuulizi pesa zake. Ndipo Mwavita anaona kuwa ni heri hata kuishi pekee yake kuliko kuwa katika ndoa ambayo haina misingi yoyote**.** Kwa mfano:

> Mwavita: Ehe kwa hivyo mke pia aliumbwa ili kutimiza haja za mume. Kwani mke hana haja zozote katika maisha? Mama basi kwa kuwa mimi nimekataa kutumiwa na Kinaya nimekuwa hasimu wa waume wote na hata wako wake wengi wanaonilaumu ati najitia uume! Kutokana kuwa mtu na kuheshimiwa, kama mtu ndio kujitia uume! (uk 77)

Mfano wa sita Mwavita anaposema kuwa "...... ehe kwa hivyo mke pia aliumbwa ili kutimiza haja za mume," umaanisho wake ni kuwa mke pia ana haki ya kushughulikiwa. Isiwe tu ni waume ambao watatarajia mengi kutoka kwa wake bila wao kuwasaidia. Hivyo basi wakati mume na mke wanapokuwa pamoja na kusaidiana na kuelewana ndoa huwa nzuri. Ikiwa hakutakuwa na kuelewana hasa pale mke atakuwa ni wakuwajibika kila wakati basi ndoa hiyo haitakuwa dhabiti.

**4.3 Umaanisho na Utamaduni**

Jamii ikiwa pamoja huwa inabuni mambo ambayo yataisaidia kukidhi utashi na maendeleo yake. Haya mambo ni pamoja na mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa maisha na taratibu zao za kuendesha maisha yao ambao ni tofauti ni jamii nyingine. Haya yote basi yakawa ndio utamaduni wa jamii ile. Katika tamthilia ya *Mama ee* kuna utamaduni wa jamii ile kwa mfano wakati Mwavita na Kinaya wanapokosana na hivyo kumfanya Mwavita kurudi

kwao, tunawaona wazee na watu wa jamii zote mbili wakiwa pamoja ili kuwakosoa na kuwaelekeza Mwavita na Kinaya, kulingana na sheria na desturi zao.Kwa mfano:

> Mzee Tembo: Babu tumekuita hapa usikize ugomvi wa hawa watoto wetu. Juzi tulikuita <u>na bure ulipotezewa wakati wako na mmoja wao kwa kutofuata.</u>
>
> Mzee wa Kijiji: Tusigombane wanangu. Ulimi huharibu na ulimi pia hutengeneza ukanyoosha iliyo kombo. Kabla ya kutizama mambo ya hawa watoto turekebishe yaliyotokea juzi katika mkutano uliofanyika papa hapa mwezi uliopita.(uk 26,27)

Umaanisho unaojitokeza katika mfano wa saba Mzee Tembo anaposema "..... na bure ulipotezewa wakati wako na mmoja wao kwa kutofuata.......," vilevile Mzee wa kijiji anaposema "...... turekebishe yaliyotokea juzi katika mkutano uliofanyika papa hapa mwezi uliopita," Umaanisho unaojitokeza ni kuwa utamaduni umo katika hatari ya kutupiliwa mbali sana na kizazi cha wasomi. Hii ni kwa sababu ni mda tu wa mwezi mmoja ambao Kinaya na Mwavita walikuwa katika kikao cha kukosolewa. Tena tunawaona wamerudi kukosolewa. Kwa ufupi utamaduni unafuatwa tu na wale wa awali kama vile wazazi wa Kinaya na Mwavita na wazee wao. Huku ukipuuzwa na kizazi cha akina Kinaya.

### 4.4 Umaanisho na Ubaguzi wa Jinsia ya Kike

Swala la ubaguzi huleta matatizo mengi katika jamii zetu. Swala hili hujitokeza kwa njia mbalimbali kwa mfano jinsia, ukabila, rangi, umri, kitaaluma, maumbile na mengine mengi. Kwa mfano:

> Mama: Ewe mtoto wa kike-umeniletea balaa na beluwa. <u>Nitafanya nini? Nitaenda wapi?</u> Ole wangu! Najuta kuzaa. Leo ndio babako <u>atatuchinja sote</u>!(uk 13)

Ni kutokana na mtuamshi ya mama "nitaenda wapi? Ole wangu? Najuta kuzaa. Leo ndio babako atatuchinja sote." Tunapata umaanisho kuwa wanawake ni wanyonge. Wamebaki wa kuonewa na kunyimwa haki zao. Ubaguzi na upendeleo unajitokeza pale ambapo ikiwa watu wawili

walishiriki kufanya kosa moja, mbona George aendelee na masomo yake ilhali ni yeye aliyempachika Tenge mimba. Mbona baba na nduguye Tenge kumuadhibu Tenge na kusahau makosa ya nduguye Tenge? Ndipo tunapata kuelewa kuwa wanawake wanachukuliwa kuwa wanyonge hivyo basi wakabaguliwa, kutengwa, kuonewa na kudhalilishwa kwa kuwa hawana wa kuwatetea.

> Baba: .......kumbe ndio hayo natija sasa! George yuko shuleni! Wewe je! (uk 15)

Maneno yake baba “George yuko shuleni wewe je!” yana umaanisho kuwa mtoto wa kike anaonewa sana katika jamii. Hii ni kwa sababu Tenge aliweza kufukuzwa shuleni ili hali George alikubaliwa kuendelea na masomo yake hata baada ya wote kufanya makosa hayo.

> Baba: wacha nimfundishe Malaya huyu apate kurejesha pesa zangu zote nizopoteza ati karo ya shule, kumbe ni karo ya kujifunza umalaya.(uk 15)

Kutokana na matamshi ya baba neno malaya lina makali sana. Wakati baba amelitumia linaleta umaanisho kuwa mtoto wa kike ni wakudharauliwa sana kiasi kwamba anapopatikana katika makosa huwa hana wa kumtetea.

> Kaka: .........nilikukanya na hilo George lako. Faida gani umepata sasa? George anasoma bado wewe je! Ulijona umesoma sana husikii unayoambiwa. Hawara mkubwa wewe.(uk16)

Kaka anapomwambia Tenge kuwa “ulijona umesoma sana...... hawara mkubwa wewe.” Tunapata umaanisho kuwa mtoto wa kike anaonewa gere hivi kwamba hamna anayemtakia kwendelea vizuri hasa katika masomo. Hii ni kwa sababu kumbe Kaka hakufurahia sana wakati Tenge alikuwa akisoma. Anaendelea kumwita “hawara” neno ambalo lina makali na ambalo lina umaanisho kuwa kuna kudharauliwa kwa jinsia ya kike na hata kuweza kuitwa majina ambayo hayafai.

> Mwavita: Si utumwa ni nini! Naleta pesa za kunua chakula. Hiyo ni kazi ya mikono yangu. Nikija chakula hicho nipike

> mwenyewe, kisipopikika
> vizuri balaa! (uk 61)

Ni kutokanan na maneno yake Mwavita " si utumwa ni nini" tunapata umaanisho kuwa mwanamke ametwikwa majukumu yote katika ndoa na hata baada ya kuyatekeleza anaendelea kuyapitia matatizo katika ndoa yake.

### 4.5. Umaanisho na Dini

Ni vigumu sana binadamu kujitenga na dini hata kama anaielewa au haielewi. Hii ni kwa sababu kila mtu ana imani juu ya mambo fulani aidha ya kibinafsi au ya umma yanayomfanya kuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu maisha. Chacha (2013), Anaendelea kusema kuwa kuna kanuni na kaida zinazowaongoza watu katika jamii zao mahususi. Kanuni hizi pamoja na miiko ni sehemu ya dini yoyote ile inayopatikana duniani. Ni rahisi mtu kujitenga na wafuasi wa dini yake kuwa kutohudhuria sehemu za ibada lakini hawezi kujitenga kamwe na dini.

Wakati mamake Mwavita alienda kuwatembelea wasichana wake Tenge na Mwavita, alikuwa anaenda kuwatuliza baada ya Mwavita kupitia mateso hadi akaamua kuwachana na mumewe na mwanawe Juma. Haya yalikuwa machungu kwa Mwavita kwa sababu mtoto wake alikuwa mdogo wa umri na ambaye alikuwa akihitaji malezi ya mama mzazi. Baada ya mazungumzo yao Mwavita alisema kuwa

> Mwavita: Wanawake wataendelea kunyonywa na kunyanyaswa na mabwana kwa kutojua haki zao. Wengi washakubali kuwa wananchi wa tabaka la chini. Ati ndivyo Mungu alivyotuumba. Wanawake kama hao mtu kama mimi huwachukua waume kama miungu. Mtu kama mimi huchukuliwa kama muasi. Nimeasi dini gani? Kuabudu waume. Simwabudu mume yeyote!(uk 77,78)

Kutokana na usemi wake Mwavita "wengi washakubali kuwa wananchi wa tabaka la chini ati ndivyo Mungu alivyotuumba," tunapata umaanisho kuwa dini imechukuliwa kuwa kipengele muhimu ambacho kinatajwa kama sehemu inayotumika kuwafanya wanawake wakubali kujisalimisha na kudhulumiwa kwa hiari yao. Utapata kuwa baadhi ya wanawake waliosoma wana mawazo sawa na ya Mwavita na mwonoulimwengu wao ni tofauti ndipo Mwavita anasema

kuwa si mume aliye adui wake bali ni wale wanawake ambao huwaabudu waume. Hao ndio hasimu wakuu kwake kwa sababu watamtafutia kila aina ya tusi kwa sababu ameasi dini yake.

Walipokuwa wakiendelea na mazungumzo yao, Padre aliingia na kushukuru kuja kwa sababu aliweza kumpata mamake Mwavita pale. Aliweza kumweleza jinsi alivyojaribu kuwashawishi Mwavita na Kinaya kurudiana pamoja bila mafanikio. Juhudi zake ziliambulia patupu kwa sababu yeye akiwa anasismama kwa niaba ya dini, alionekana kuegemea upande mmoja. Hatumwoni akimshawishi Kinaya. Ajapo kwa Mwavita, anamwambia kuwa warudiane na mumewe kwa kuwa ndoa yao ilikuwa ya Sakramenti ya kanisa. Hasemi makosa ya Kinaya kwa sababu ni mwandani wake wa chanda na pete ambaye hushiriki naye ulevini. Kwa vile amevalia tu joho la dini basi anataka kila mtu amchukulie kuwa yeye ni mcha Mungu halisi. Tenge wanakosana na yeye na hapo ndipo alimwambia ukweli kuwa:

> Tenga: Tuambie jingine Padre wa Mungu! <u>Alikununulia chupa ngapi</u>? Na Mwavita akirudi atakununulia ngapi zaidi.(uk 83)

Kutokana na maneno yake Tenge "alikununulia chupa ngapi?" kuna umaanisho kuwa dini pia ni ya kuegemea upande mmoja na ni ya kutumika tu na watu kuficha hali zao za kawaida. Kama vile Padre ambaye anatambulika kuwa mlevi sana. Mwavita naye akawa na shaka kuwa ukiwa yeye Padre hajaoa ataelewa vipi mambo ya ndoa akaweza kumshauri Mwavita! Tunatambua pia kuwa Padre mmoja huyu ambaye anamwambia Mwavita amsamehe mumewe, na waweze kurudiana, mbona yeye kama Padre asimsameha Mwavita hadi akamtoa kwenye kushiriki katika komonio akisingizia kuwa Mwavita ni mwenye dhambi. Tunaona kuwa pia Tenge, Padre amekataa kumpa mtoto wake ubatizo kwa kusingizia kuwa ni mwanaharamu. Hapo dini inaleta utata. Je, anaweza pia kumkataza Kinaya kutoshiriki komunio.

> Padre: Sheria ya kanisa inasema mume na mke huwa mtu mmoja wakioana. Na Mungu alisema katika Bibilia kuwa mwanadamu yeyote asiwatenganishe wawili aliounganisha Mungu kuwa mwili mmoja na roho moja. Hata wewe mwenyewe Mwavita huna madaraka ya kujitenganisha na Kinaya. Unavunja sheria ya Mungu na…….(uk 82)

Umaanisho unaojitokeza ni kuwa sheria za dini zimelegeza msimamo wake katika masuala ya ndoa. Hazitoi maelezo kamili kuhusiana na ndoa pale ambapo mwanamke ataona kuwa anahatarisha maisha yake ikiwa ataendelea kukaa katika ndoa inayoyumba. Umanisho mwingine ni kuwa mwanamke aliyetengana na mumewe huchukuliwa kuwa mkaidi mjini. Hukataliwa na wanawake wenzake ambao kwao huona wako sawa katika dini ya utumwa na waume zao. Dini humtenga mwanamke kama hivyo na kumuona kuwa aitwe muasi kuliko kuishi katika utumwa. Tenge naye amekataliwa na dini kwa sababu ya kkuzaa nje ya ndoa wanawake hawa wawili dini inawaona kwa mtazamo hasi. Wanachukuliwa kuwa waasi na wasiofaa kutangamana na wenzao.

Howard (2011) katika kazi yake, anasema kuwa dini ni sehemu moja ya utamaduni wa watu, lakini dini ambazo zilikuja zina ubepari mwingi. Hii ina maana kuwa dini ni mojawapo ya asasi ambazo zinawakandamiza wanawake. Kwa mfano, wakati ambapo Kinaya na mkewe wanapokosana, juhudi za Padre zinagonga mwamba za kuwaleta pamoja kwa sababu ya kuegemea upande mmoja wa Mwavita.

Umaanisho unaojitokeza ni kuwa iwe dini ya awali au ya kisasa, hakuna ile ambayo ina usawa. Dini inatumika kuwakandamiza wanawake ambao wamebaki kuwa watumwa wa dini hizo ambazo ni za kuwalaumu, kuwatenga na kuwadhulumu wanawake.

### 4.6 Umaanisho na Ushirikiano wa Akina Mama

Umoja wa kina mama ni jambo ambalo hukumbwa na pingamizi kali. Wanajamii huwaona wale kina mama ambao wanatetea uhuru wao kama kundi la wanawake waasi ambao wametengana na tamaduni za kijamii. Hilo jambo huwa halina msingi wowote kubainika kuwa kila mtu ana haki ya kutetea uhuru na maslahi yake. Wakati mume na mke wanapoamua kutengana huwa kuna mambo ambayo huibuka na kuwalazimu kuchunguza tena kauli au uamuzi waliochukua. Kwa mfano katika ndoa iliyo na watoto huenda wazazi wakaamua kurudiana kwa kuzingatia malezi ya watoto wao. Wao hurudiana pasi na masharti wala mpatanishi yeyote.

Wakati Kinaya alipomtembelea Mwavita baada ya kuwachana, alikuwa amesukumwa na wazo kuwa mtoto wake Juma alikuwa anahitaji malezi ya mama yake. Alipofika katika makazi yao walikohamia, aliingia ndani ya nyumba na kumrahi Mwavita warudiane naye kwa sababu ya Juma. Mwavita hakupendelea sana kutajwa kwa mwanawe Juma. Kinaya alipohonga korti akapewa mtoto Juma, alifikiri kuwa Mwavita kwa kumkosa mwanawe ataamua kurudiana na

yeye bila kushawishiwa na yeyote. Hilo halikuwa akilini mwa Mwavita. Kinaya alishangazwa kugundua kuwa Mwavita hakushawishiwa kwa kumwacha mtoto wake. Katika hali hiyo, Mwavita walishirikiana na Tenge kwa  kumwadhibu Kinaya. Alipewa kichapo cha mbwa hadi akararuliwa nguo zake zote akabaki na chupi peke yake. Umoja wa wanawake wake hawa wawili umejidhihirisha.

Kwa mfano:

Tenge: Ha,ha,ha! <u>Kweli leo tumemweza.</u> Siku zote atutilia fujo hapa. Polisi hawafanyi lolote. Ndio akafura kichwa aona sisi wake hatuna msadidizi basi aweza kufanya lolote atakalo hapa.

Mwavita: Naomba hao polisi waje watusaidie twende mahakamani tena tuwatie aibu. Tutasema yote, tumeripoti mara nyingi. Wao hawafanyi kitu. Hongo tu!(uk 122)

Kutokana na kauli hii “Ha, ha, ha kweli leo tumeemweza siku zote atutilia fujo hapa.” Umaanisho unaojitokeza ni kuwa kusiwe na vipangamizi vyovyote katika maisha ya mwanamke ambavyo vitafanya kutotetea haki yake na kutafuta uhuru wake. Umoja huu unarejelea katika ngojera ya ‘umoja wa kina mama’ ambayo inapatikana katika utangulizi wa tamthilia hii. Umoja ndicho kiini kikuu katika kuungana kwa kina mama. Bila umoja basi akina mama watapitia hali ngumu ya maisha kwa sababu hawatakuwa na wa kuwatetea.

Baada ya vita hivi, Tenge na Mwavita waliamua kwenda katika ofisi ya chama cha kina mama. Walipofika katika ofisi ambayo ilikuwa imepambwa ikapambika waligundua kuwa chama cha umoja wa kina mama kipo lakini umoja wenyewe ulikuwa haupo. Idadi ya wanawake wasomi ni chache na ni ya wale wapatikanao mijini. Wengi ni wale kina mama walioko vijijini na amabao si wasomi. Hii ina maana kuwa ikiwa wanawake wa mijini na vijijini wataungana pamoja katika kupigania haki zao basi bila shaka watapata mafanikio.

**4.7 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia jinsi umaanisho unavyosaidia kuibua maudhui katika *Mama ee.* Katika kulitathmini lengo hili, utafiti huu uliweza kujumlisha matumizi ya lugha na mazungumzo ya wahusika na kuweza kubaini kipengee ambacho kinazua umaanisho, ambao hatimaye unaongoza

katika kuibua maudhui. Hivyo basi utafiti umedhihirisha kuwa umaanisho umesaidia kuibua maudhui katika *Mama ee*.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Baada ya kukamilisha utafiti huu na kuchanganua data katika sura ya pili, tatu na ya nne, sura hii inatoa mukhtasari wa tasnifu nzima na kufafanua iwapo malengo ya utafiti huu yaliafikiwa au la. Katika sura hii, pia tunamulika mapendekezo kuhusu tafiti zijazo katika suala la umaanisho hasa katika riwaya, hadithi fupi na mashairi.

### 5.2 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kubainisha iwapo umaanisho umejitokeza katika *Mama ee,* jinsi umaanisho huo unavyosaidia kuhakiki ujenzi wa wahusika katika *Mama ee* na mwisho kutathmini ni kwa jinsi gani umaanisho umechangia katika kukuza maudhui katika *Mama ee.*

Lengo la kwanza la utafiti huu ni kubainisha iwapo umaanisho unavyojitokeza katika tamthilia ya *Mama ee* limeafikiwa. Tamathali zilizochunguzwa ni pamoja methali, sitiari, jazanda, majazi, tashbihi kisengere nyuma na kejeli. Matumizi haya ya lugha bila shaka hayakupachikwa tu kiholelaholela katika tamthilia ya *Mama ee.* Matumizi yake yanaweza kuzua umaanisho ambao umesaidia kuelewa kazi. Nimeweza kuteua matumizi haya ya lugha na mhusika ambaye aliyasema na kubaini maana yake ambayo inaleta umaanisho. Matumizi haya ya lugha kwa mfano yana maana yake katika kamusi ya methali na misemo. Kando na maana hizo, niliweza kuibua maana na jinsi vile zilivyotumiwa na wahusika mbalimbali katika *Mama ee.* Sitiari ni nyingi mno. Kando na zile zinazotambulika katika vitabu vya Kiswahili.

Matumizi ya jazanda pia yameshughulikiwa na kutolea maana kulingana na vile zimetumika katika tamthilia hii. Majazi, kisengere nyuma pia ni matumizi ya lugha ambayo nimeyashughulikia ya lugha yanayozua umaanisho katika tamthilia ya *Mama ee*. Kwa vile matumizi hayo hayakupachiswa tu katika mchezo huu, hiyo ndiyo ilikuwa sababu ya kufanya uchambuzi wa ndani na kuibua umaanisho uliolengwa katika kazi hii.

Matumizi haya ya lugha yameweza kuzua umaanisho kwa sababu katika matumizi yake, nyingi zimekiuka kanuni ya ukweli, uhusiano, namna na idadi. Hivyo basi kwenda kinyume na

alivyosema Grice kuhusu utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo. Katika kukiuka kanuni hizo basi utafiti umedhihirisha kuwa umaanisho umejitokeza katika tamthilia ya *Mama ee.*

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi ambavyo ukiushi wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano unavyosaidia kuhakiki ujenzi wa wahusika katika *Mama ee*. Imebainika kuwa, kuna uhusiano mkubwa sana baina ya ukuzaji wa sifa za wahusika wakuu aidha kwa kuzingatia au kukiuka kanuni za umaanisho kulingana na Grice. Katika sura hii ya tatu imethibitishwa kuwa sifa za wahusika ambao ni Mwavita, Kinaya, Tenge, Mama, Baba, mzee wa kijiji, Ba mkubwa Kinaya, Nyanya na Kaka ya Tenge, zinabainika kutokana na kuvunjwa kwa kanuni za utaratibu wa ushirikiano katika mazungumzo yao. Ukiushi huu kwa unazua umaanisho ambao unatuongoza kufasiri uhusika wa wahusika hawa katika tamthilia ya *Mama ee.*

Kwa sababu pia ya heshima aliyonayo kwa wazazi, nyanya na wakwe zake na hata wazee wa kijiji, pia tunamwona akivunja zile kanuni, ili isionekane kuwa hapimi maneno yake. Kinaya kwa upande wake kutoka mwanzo hadi mwisho ameonekana kuvunja zile kanuni nne. Hii ni kwa sababu anajaribu kuficha uso wake ili watu wasije wakamuona mbaya baada ya kumtendea Mwavita mabaya hayo yote. Kinaya hajaweza kuweka usemi wake waziwazi hivyo basi matendo yake yakawa yanaenda sambamba na sifa zake hivyo kulandana vizuri na jina lake la kimajazi Kinaya.

Ili mhusika aonekane kuwa yeye hana heshima, atakuwa amekiuka kanuni za utaratibu wa ushirikiano hivyo basi kuzua umaanisho. Katika kushughulikia lengo hili la pili, utafiti huu umeweza kumchunguza kila mhusika na mazungumzo yake na kutoa kipengee muhimu ambacho kinaonyesha kukiukwa kwa kanuni za utaratibu wa ushirikiano hivyo basi kuweza kutoka umaanisho unao jitokeza na kuweza kuwasawiri wahusika hao. Katika kutathmini lengo hili la pili, utafiti huu umebaini kuwa umaanisho unaweza kutumika kuwasawiri wahusika katika tamthilia ya *Mama ee.*

Lengo la tatu linachunguza jinsi umaanisho umechangia katika kukuza maudhui katika *Mama ee*. Maudhui ambayo yamejitokeza ni pamoja na mgogoro katika ndoa, utamaduni, ubaguzi wa kijana wa jinsia ya kike, sheria na umoja wa wanawake . Yaliyochangia kubainisha maudhui haya ni pamoja na matumizi ya lugha na wahusika na uhusika wao katika mchezo mzima.matokeo ya utafiti huu ni kuwa sitiari zimechunguzwa na kubaini kuwa kando na maana

zilizotolewa katika kamsi kuna vile zinavyotumika na kuleta maana ya ndani. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa kwa kuchukulia umaanisho kwa ujumla, utafiti huu umebaini kuwa kuna maudhui ambayo yamejengwa kutokana na matumizi ya lugha ambayo yameshughulikiwa katika lengo la kwanza. Pia wahusika na uhusika wao ambao umejidhihirisha kutokana na mazungumzo yao, kwa kuvunjwa kanuni za utaratibu wa ushirikiano, kumesaidia kukuza maudhui katika *Mama ee.*

### 5.3 Mapendekezo

Kwa sababu ya muda na kujikita kwangu katika kufanya utafiti kuhusu mada ambayo imeshughulikiwa, ninapendekeza tafiti zifuatazo zifanywe. Kwanza ni utafiti utakaochunguza suala la Umanisho katika tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile riwaya na hadithi fupi ili kubainisha jinsi ukiushi wa kanuni za utaratibu wa ushirikiano unavyoibuka ili kutoa maana ya msemaji. Vilevile ninapendekeza watafiti wengine waweze kuchunguza Umaanisho katika miktadha mbalimbali kama vile harusi, jandoni na matanga ili kubaini jinsi unavyojitokeza na hivyo kulenga maana ya msemaji.

### 5.4 Hitimisho

Katika sura hii, muhtasari wa yale ambayo yameshughulikiwa katika utafiti huu yameelezwa. Malengo ya utafiti huu yameweza kutimizwa, mapendekezo ya tafiti zingine yameelezwa.

## MAREJELEO


Arege M. na Nyanje M. (2011). *Kamusi fafanuzi ya Methali.* Nairobi : Target Publishers.

Blutner, R. (1998). "*Lexical Pragmatics in Journal of semantics"* Vol. 15 (2) pp 115-162.

Chacha, W.C. (2013). "Taswira ya mwanamke katika tamthilia ya nguzo ya Mama ee." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Crystal, D. (2003). *The Cambridge Encyclopaedia of English Language 2nd Edition.* Cambridge: Cambridge University Press.

Darighgoftar, S., (2012). "Different Homeophathic Characters violate Cooperative Principles Differently." *International Journal of Linguistics.* 4, 266-280.

Grice, H. P. (1975). *Logic and Conversation: Philosophy of Language*. New York: Oxford University Press.

Habwe, J.H. (2011). *The Discourse of Political Language in Kenya*: UK LAP LAMBERT Academic Publishing: Germany. Academic.

Kerubo A.O. (2013). "Uwazi na Umaanisho. Usimbaji maana kimazungumzo katika Ekegusii na Kiswahili." Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kuhenga C. (1977). *"Tamathali za usemi:* Dar es salaam: East Africa Literature Bureau.

Lackoff, R. (1976). *Language and Society in a Survey of Applied Linguistics.* Michigan: University of Michigan Press.

Malmkjaer, K. (2004). *Translation in Undergraduate Degree Programms.* Amsterdam Philadelphia.

Mey,L. (2001). *Pragmatics: An Introduction.* U.S.A. Blackwell Publishers Ltd.

Mekacha,R.,D., K. (2004). *Nadharia ya Muktadha wa Kiswahili.* Tuki. Dar es Salaam.

Mugenda na Mugenda. (1999*). Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mulokozi. M., (1996), "Utangulizi wa Fasihi simulizi ya Kiswahili. Dar es salaam. East Africa.

Ngoge, A.T. (2012). "A relevance Theoritical analysis of Implications in Ekegusii. Idioms- A

case Of Communication in Kiobegi Market: U.O.N. Tasnifu ya M.A.

Njuguna (2010) "*Manifestation of Stereotypes through Gikuyu Figurative Language.*" University of Nairobi.

Ogola, C. A. (2006) *Apragmatic Analysis of International Communication Failures.* Tasnifu ya M.A.

Okuku, M. (2010). Uchanganuzi wa kiisimu baadhi ya matini ya Kiswahili: Mtazamo wa Pragmatiki Leksika. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Onyoni, J.K. (2012). *Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Natala na Mama ee. Tasnifu ya M.A.* Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwachofi, A., K. (1987). *Mama ee:* Nairobi: EAEP.

Trudgil, P. (1983). *Sociolinguistic typology and Complexification. New York.* Oxford University Press.

Wafula, R. na Kimani, N. (2007). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publishers.

Yule (2010): *The study of Language 4th Edition*: Cambridge; Cambridge University Press.